**Wanaharakati**, wanasiasa walia kusiginwa Sheria ya Vileo Zanzibar

UKURASA 3



**Bunge** lashtuka utitiri mifuko ya uwezeshaji wananchi

UKURASA 3

MSAKO SIKU 189...

**Maneno** matamu yatumika kumnasa aliyetoroka akiwa mahabusu ya polisi

UKURASA 4


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Milipuko wa mimba utotoni makambi wakimbizi UNFPA, Japan waungana
Hospitali Bugando katika mapinduzi ya tiba vichwa vikubwa, mgongo wazi
MMAM & SAFARI YA 2030 SDGS...
Rais anavyopambana na Wizara Afya tija wodini, kupunguza vifo
• Mwanza, Arusha watangaza nuru vituo afya

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Februari 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0581580

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Lissu azuiwa redioni, Nape atoa neno




• **Ni** utata ulioibuka mahojiano yake kupigwa 'stop', watangazaji waanika.... *Endelea Ukurasa 2*



## Samia kuwalipia pasipoti madereva wote wa malori

• **Makonda** amrejeshea mama nyumba aliyopokwa na UWT... *Endelea Ukurasa 3*

## Sajenti Polisi jela maisha kwa kulawiti mwanawe

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akitia saini kitabu cha maombolezo kutokana na kifo cha Rais wa Namibia, Hayati Dk. Hage Geingob, katika Ofisi za Ubalozi wa nchi hiyo, Masaki, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** GAMONDI: MUHIMU POINTI TATU UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Lissu azuiwa redioni, Nape atoa neno

**Elizabeth Zaya na Paul Mabeja**

KUMEIBUKA utata kuhusu kuahirishwa kwa mahojiano kati ya Tundu Lissu na watangazaji wa Wasafi Media, mwenyewe akifunga safari hadi kwenye studio za chombo hicho cha habari jijini Dar es Salaam akitaka aelezwe nani aliyetoa agizo la zuio hilo.

Kukiwa na utata huo, serikali kupitia Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, imesema haihusiki na kuzuiliwa kwa mahojiano hayo yaliyopangwa kufanyika jana kwenye Kituo cha Redio cha Wasafi FM.

Jana asubuhi, kulisambazwa taarifa kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii kuwa Lissu ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alifika kwenye studio za Wasafi FM akitaka apewe sababu kwanini kipindi chake kilizuiliwa kufanyika.

Ilioneshwa watangazaji wa kituo hicho wakithibitisha walikuwa na ratiba ya mazungumzo na Lissu, lakini kutokana na kwa sababu zilizo nje ya uwezo wao, kiliondolewa.

"Jana (juzi) hapa tulikuwa tumekubaliana tungekuwa na Tundu Lissu, lakini kwa bahati mbaya sana, kwa sababu ambazo ziko nje kabisa ya uwezo wetu, ile 'interview' (mahojiano) ikawa imekuwa 'cancelled' (imefutwa) jana (juzi) jioni kabisa.

"Lakini Tundu Lissu mwenyewe kwa bahati mbaya alisema hakuridhika na hakupata sababu za kutosha," alidai mmoja wa watangazaji wa kiume wa kituo hicho.

Ilidaiwa kuwa Lissu alifika katika ofisi za chombo cha habari hicho saa 10 alfajiri na akakaa kwa zaidi ya saa tatu, akisubiri kupatiwa sababu za kuzuiwa kwa mazungumzo yao redioni.

Baadaye Lissu alifanikiwa kufanya mazungumzo na uongozi wa kituo hicho na akaweka wazi baadhi ya waliyozungumza ofisini.

"Nilipopata mwaliko ule, nilikuwa na wasiwasi kidogo kwa sababu ninafahamu kwamba masuala ya vyombo vyetu vya habari yamekuwa na matatizo kwa miaka kadhaa sasa.

"Kwahiyo, nilikuwa na shaka kwamba kweli hawa wataweza kukubali nije kwenye kipindi chao? Lakini walinitoa hiyo shaka kwamba 'tumezungumza na wakubwa wetu, mambo yote yako sawa, Mheshimiwa usiache kuja'.

"Jana (juzi) usiku, nikapata habari kwamba kipindi kimechomolewa (mahojiano yao yamefutwa). Nikauliza 'kwanini?' Jibu nililopewa ni 'maagizo kutoka juu'.

"Nikasema 'nitakuja asubuhi na mapema kuja kuuliza ili nithibitishiwe kama yale mambo ya maagizo kutoka juu tuliyokuwa tunafikiria bado yapo'. Kwahiyo, ndicho kilichonileta hapa," Lissu alisema.

Msomi huyo wa sheria alisema kuwa baada ya kuzungumza na uongozi wa kituo hicho, aliridhika pasi na shaka na sababu alizopewa.

"Nimezungumza na viongozi wa Wasafi TV, wamenihakikishia kwamba kipindi hakijachomolewa kwa sababu ya maagizo kutoka juu, bali kulikuwa na matatizo ya mawasiliano miongoni mwa waandaji wa kipindi pamoja na menejimenti kwa namna ambayo kipindi kisingekuwa bora.

"Na nilivyopata hayo maelezo nimewaambia, na ninaomba niseme hii kwamba sina sababu yoyote ya kutokuwaamini, kutokuamini maneno yao.

"Wamesema ni kwa sababu ya hayo mawasiliano kutokuwa sawa miongoni mwao si kwa sababu za maagizo kutoka juu na tumekubaliana kwamba tutafute muda mwafaka wafanye maandalizi wanayoona yanastahili ili nije kufanya kipindi katika siku zijazo. Ndicho ambacho ningependa kukisema kwa hatua ya sasa," Lissu alisema.

**KAULI YA WIZARA**

Katika tamko lake la jana jijini Dodoma kuhusu suala hilo, Nape mbali na kusema serikali haihusiki na kilichojiri, aliutaka uongozi wa Wasafi Media useme ukweli kuhusu kilichotokea mpaka mahojiano hayo kutofanywa.

Waziri huyo alisema kuwa tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani (Machi 19, 2021), serikali imefanya mambo mengi mazuri kwa tasnia ya habari.

"Rais pia amehakikisha kuwapo demokrasia nchini ikiwamo uhuru wa watu wote kuzungumza bila kuzuiwa, wakiwamo viongozi wa vyama vyote vya siasa na aliagiza kuangalia ustawi wa vyombo vya habari kiuchumi na kuandaa kamati ya kutathmini hali ya uchumi wa vyombo hivyo.

"Kutokana na nia yake hiyo njema ya Rais, hakuna uwezekano wa maelekezo yoyote ya kuingilia uhuru ambao amekuwa akiamini na kujenga kwa vyombo vya habari nchini," alisema.

Waziri Nape pia alisema serikali imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari kama dira yake ya kuendeleza dhana yake nzima ya 'Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Utaifa, yaani 4R)'.

Alisema serikali itaendelea kulinda uhuru wa vyombo vya habari na akavitaka vyombo hivyo kutoa nafasi kwa vyama vyote vya siasa bila upendeleo hasa wakati huu kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

# Sajenti Polisi jela maisha kwa kumlawiti mwanawe

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Singida imemhukumu kifungo cha maisha gerezani askari polisi mwenye cheo cha sajenti, David Sangan, baada ya kupatikana na hatia ya kulawiti mwanafunzi mwenye umri wa miaka saba ambaye ni mtoto wake.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Fadhiri Luvinga baada ya mahakama kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na askari, walimu na daktari aliyefanya vipimo kwa mtoto huyo na kubaini mwanafunzi huyo wa kiume alikuwa anafanyiwa vitendo hivyo.

"Kwa kuzingatia uzito wa ushahidi uliotolewa mahakamani hapa na mashahidi, ukiwamo ushahidi wa mtoto mwenyewe, mahakama hii imeridhika pasi na kuacha shaka yoyote kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume cha sheria.

"Hivyo, mahakama inakuhukumu kifungo cha maisha gerezani ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia hii," alisema.

Jeshi la Polisi nchini lilishamchukulia hatua za kijeshi askari huyo ambaye alikuwa dereva wa jeshi hilo ikiwamo kumfuta kazi.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 35 ya mwaka 2023, askari huyo alidaiwa kumwingilia kinyume cha maumbile mwanafunzi huyo, jambo ambalo ni kosa mujibu wa Kifungu 154(1) na (2) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16 ya Mwaka 2022.

Kabla ya hukumu hiyo, Mawakili wa Serikali Sara Amandus na Caren Rwebangila, walidai mahakamani kuwa mshtakiwa huyo alikuwa anatenda kosa hilo kati ya Oktoba 2021 na Machi 18, 2023, eneo la Utemini katika Kota za Polisi, Kata ya Ipembe, wilayani Singida.

Ilidaiwa mahakamani kuwa mwalimu wa darasa katika Shule ya Msingi Utemini, Manispaa ya Singida ndiye aliyegundua tatizo la mtoto kufanyiwa ukatili baada ya kuona maendeleo yake darasani yanashuka.

Ilidaiwa kuwa mwalimu huyo alibaini mtoto huyo kila alipokuwa anakaa darasani, kaptura yake ilikuwa inatoa uchafu na haja kubwa, ndipo mwalimu huyo akamweleza Mwalimu Mkuu wa Shule ambaye alitoa taarifa polisi.

Katika ushahidi wao, mashahidi hao walidai kuwa baba wa mtoto huyo ambaye ni askari polisi, wakati anafanya kitendo hicho cha kikatili, alikuwa akimtishia mwanawe kumuua kwa kumpiga risasi iwapo angetoa taarifa za ukatili huo.

Vilevile, ilidaiwa kuwa uchunguzi uliofanywa na daktari, ulibaini kuwa haja kubwa ilikuwa inamtoka mwanafunzi huyo bila mpangilio. Pia alikuwa na michubuko sehemu ya haja kubwa na tundu la haja kubwa lilikuwa wazi, likipanuka kwa sentimeta tatu.

Kabla ya hukumu hiyo, mshtakiwa aliiomba mahakama iahirishe kusoma hukumu kwa kuwa alikuwa anaumwa, ombi ambalo lilipingwa na mawakili wa serikali waliodai mshtakiwa atoe vielelezo kama kweli ni mgonjwa.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa mahakamani huko kwa mara ya kwanza Desemba 21, 2023.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 154(1) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, mtu yeyote ambaye anamuingilia mtu yeyote kinyume cha maumbile au anamwingilia mnyama kimwili au anamruhusu mwanamume kumwingilia yeye mwanamume au mwanamke kinyume cha maumbile, atakuwa ametenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha na wakati mwingine kifungo kisichopungua miaka 30 gerezani.

Sheria hiyo inatamka katika kifungu 154(2) kwamba "ikiwa kosa limetendwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki dhidi ya mtoto wa umri wa chini ya miaka 10, mkosaji atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha."


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
08.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Ijumaa tarehe **09-02-2024 hadi 12.02.2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar- Es- Salaam Port kuelekea Mzenga,** gari hiyo ina namba ya usajili: **T 163 DFE / T 310 DDH**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 7.00**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar-Es-Salaam hadi Mzenga** kupitia **Morogoro Road** Gari itasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar- Es- Salaam Port mpaka Mlandizi** Kutoka **Mlandizi kwenda Mzenga** gari itasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
08.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Ijumaa tarehe **09-02-2024 hadi 12-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam kuelekea Kilombero** kupitia **Mikumi** gari hizo zina namba za usajili: **T 868 DXS /T 630 AJA, T 973 DTN /T 273 DUH, T 918 DSD /T 269 DUH, T 308 EDD /T 272 DUH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 5.20**
   **Kimo - mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## HABARI KITAIFA

# Samia kuwakatia pasipoti madereva malori

**Na Beatrice Shayo**, SONGWE

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kuwalipia hati za kusafiria madereva wote wa malori wanaosafirisha mizigo kwenda nchi jirani ili kuwarahisishia kuingia bila kikwazo.

Katibu wa halm ashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anayeshughulikia Uenezi, Itikadi na Mafunzo, Paul Makonda, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika mji mdogo wa Mlowo mkoani hapa.

Alisema kutokana na madereva kutokuwa na hati za kusafiria kama walivyomweleza , Rais Samia amekubali kuwasaidia.

"Madereva wengi wa malori wanaopeleka mizigo Zambia, Malawi, Congo na nchi zingine hawana pasipoti zile kubwa, hivyo wanakata zile za muda lakini wanagongewa halafu hawaruhusiwi.

"Nikamtafuta Mwenyekiti wetu wa Chama (Rais Samia) nikamwambia madereva wako wa malori wanatakiwa kuwa na pasipoti na wengi wao hela zao si nyingi ni za kuchanga, wanapambania maisha na masharti waliyopewa wanatakiwa kuwa na pasipoti kubwa ambayo kulipia ni gharama kubwa dereva mpaka ajichange adundulize hizo fedha," alisema.

Makonda alisema kwa upendo wa Rais Samia alimweleza awajulishe madereva wote wa malori wanaosafirisha mizigo na kwa sababu ameamua kupanua bandari watapata kazi nyingi.

"Ninazo habari njema kwa madereva wa malori nchini kwamba Rais Samia atatoa mchango wake kwenu kuhakikisha mnakamilisha nyaraka kama kitambulisho cha taifa au cheti cha kuzaliwa kwa mujibu wa masharti ya kupata pasipoti," alisema Makonda huku akibainisha kuwa fedha atazilipa ili madereva wapate hati za kusafiria na kufanya kazi kwa maendeleo ya familia zao na taifa kwa ujumla.

Awali madereva wa malori walieleza kukabiliwa na tatizo la kukosa hati za kusafiria ambazo wanazikata za muda mfupi na wanapofika katika mipaka wanajulishwa hazisomeki vizuri na wakiwaomba wafanye mawasiliano kujiridhisha, hawataki na kuwataka warudi Dar es Salaam, jambo ambalo linawapotezea muda.

# Wanasiasa, wanaharakati walia kusiginwa sheria vileo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANASIASA na waharakati Zanzibar, wamesema Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar imevunja sheria ya mwaka 2020 kwa kuwapa vibali waingizaji ambao si Wazanzibari kinyume cha masharti ya sheria hiyo.

Wakizungumza na waandishi wa Habari mjini hapa jana, walisema kwa mujibu wa Sheria ya Vileo ya mwaka 2020 kifungu cha 33 kilichopitishwa na Baraza la Wawakilishi, waingizaji wa vileo wanatakiwa wawe watatu na sharti lazima wawe Wazanzibari.

"Bodi ya Vileo imevunja sheria na inawaumiza wawekezaji wazalendo katika sekta hiyo wakiwamo wanaofanya biashara ya pombe kwa zaidi ya miaka 30 Zanzibar," alisema mtaalamu wa masuala ya fedha na Uchumi. Abdulahamid Mshangama.


Alisema ili kunusuru sekta ya utalii, waziri mwenye dhamana katika vibali vya uingizaji wa vileo, atafakari upya matatizo yaliyojitokeza baada ya uhaba mkubwa wa pombe kujitokeza katika hoteli na waathirika wakubwa wakiwa watalii kutoka nje ya nchi.

Mshangama alisema hivi sasa wamiliki wengi wa baa wanakimbilia katika kambi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kutafuta vileo lakini kiwango kinachoingizwa ni kidogo na tatizo kuendelea kubaki kubwa.

"Kiuchumi litatuyumbisha sana ingawa mwezi unaokuja ni mwezi wa mfungo wa Ramadhani. Baada ya hapo tutaingia katika msimu wa utalii na madhara yake tutayaona kwa sababu wageni wanaoondoka wanabeba sifa si nzuri ya kuitangaza Zanzibar," alisema Mshangama.

Mbunge wa zamani waa Kikwajuni, Paramuk Sigh Hoogan, alisema pato la taifa la Zanzibar asilimia 90 linategemea sekta ya utalii na kwamba ni muhimu serikali ikatatua tatizo lilojitokeza.

"Kuwanyima watu vibali hivi juzi nasikia moja kati ya wawekezaji wakubwa amepata mshtuko ya maradhi ya moyo na kulazwa katika hospitali ya Global kabla ya kuhamishiwa hospitali ya Aga Khan wakati wafanyabiashara wazawa wamekuwa wakifanya biashara hizo kwa miaka mingi Zanzibar," alisema.



Mwanasiasa mkongwe, Baraka Shamte



Aliyekuwa Mbunge wa zamani jimbo la Kikwajuni, Paramuki Singh Hogan

Alisema wakati umefika serikali kupitia upya Sheria ya Vileo kuruhu soko huru ili kampuni ziruhusiwe kuingiza na serikali ifanye kazi ya kukusanya kodi badala ya kuweka masharti ya kampuni tatu kuingiza pombe.

Mwanasiasa mkongwe Zanzibar na mtoto wa Waziri Mkuu wa kwanza wa Zanzibar, Baraka Mohamed Shamte, alisema matatizo yanayojitokeza Zanzibar yanatokana na kuondolewa kwa azhimio la Arusha baada ya kuwapo baadhi ya viongozi kujishirikisha na biashara huku wakiwa na dhamana ya uongozi.

Alisema inasikitisha Zanzibar ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufichua ufisadi lakini hakuna watu wanaochukuliwa hatua za kukamatwa na kufikishwa mahakamani jambo ambalo ni kinyume cha msingi ya utawala wa sheria.

"Viongozi wamekuwa walafi kwa kuiba mali za umma na hilo ni tatizo. Imewekwa ZAECA makusudi kuwadhibiti wezi nambie nani kachukulliwa hatua,"alisema Shamte ambaye amekuwa mkosoaji mkubwa wa serikali.

Hata hivyo, alisema kitendo cha Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, kujiuzu kimeonyesha ujasiri mkubwa kwa vile kimelenga kulinda maslahi ya taifa na kuendeleza mendeleo ya sekta ya utalii ambayo ndiyo nguzo ya Uchumi wa Zanzibar.

Simai alijiuzulu takriban wiki mbili zilizopita baada ya kampuni tatu za wazawa kunyimwa vibali vya kuingiza pombe na kupewa kampuni za kigeni jambo ambalo limesababisha uhaba mkubwa wa pombe na kuathiri sekta ya utalii na upatikanaji wa vileo katika nyumba za starehe na burudani visiwani hapa.

## Bunge lashtushwa na utitiri wa mifuko uwezeshaji kiuchumi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

UTITIRI wa mifuko ya uwezeshaji wananchi, ambao umesababisha ufanisi mdogo na kukosa tija, umeliamsha Bunge na kuazimia mambo mawili mazito, ikiwamo kuitaka serikali kufanya tathmini ya haraka itakayoiongoza kuunganisha mifuko yote na kubaki na michache.

Kati ya mifuko hiyo, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ambao bajeti yake haijatolewa kwa takribani miaka mitano, hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana. Imo pia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, ambayo inatishiwa na ufinyu wa bajeti.

Akiwasilisha jana Bungeni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu shughuli za kamati hiyo kwa Mwaka 2023, Mwenyekiti wake, Fatma Tawfiq, alisema kutokana na wingi huo wa mifuko, kamati inaona imekosa ufanisi, hivyo kushindwa kufikia tija iliyokusudiwa.

"Kwa kuwa bajeti inayotengwa na serikali kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kila mwaka ni ndogo, na vilevile bajeti hiyo haijatolewa kwa takribani miaka mitano na kusababisha kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana;

"Na kwa kuwa, uwepo wa mifuko mingi ya uwezeshaji wananchi unasababisha ufanisi wa mifuko hiyo kukosa tija iliyokusudiwa, Bunge linaazimia serikali iongeze bajeti na kutoa fedha inayoidhinishwa na Bunge kila mwaka, na kwa wakati ili kukukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana.

"Kufanya hivyo, kutasaidia kufikia malengo na tija iliyokusudiwa. Aidha, serikali ifanye tathmini itakayosaidia kuona umuhimu wa kuunganisha mifuko yote ya uwezeshaji wananchi, na kuingushanisha. Lengo ni kuwa na mifuko michache, ambayo itawezesha vijana kupata ujuzi na kuwezeshwa kimitaji ili kuwa na tija endelevu kwa wanufaika," alisema

**DENI SERIKALI PSSSF**

Kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Tawfiq alisema licha ya Rais Samia Suluhu Hassan kufanya uamuzi wa kulipa Sh. trilioni 2.17 kupitia hati fungani maalumu, ikiwa ni sehemu ya deni la sh. trilioni 4.6, bado serikali inadaiwa sh. trilioni 2.45

"Kamati inampongeza Rais, Samia Suluhu Hasan, kwa kufanya maamuzi ya kulipa madeni ya muda mrefu ya kiasi cha shilingi trilioni 2.17 kupitia hati fungani maalumu ikiwa ni sehemu ya deni la shilingi trilioni 4.6.

"Madeni hayo yanajumuisha madeni ya michango ya wanachama, mikopo ya miradi, ambayo mifuko iliyounganishwa iliikopesha serikali. Ni matumaini ya kamati kuwa serikali italipa deni lililobaki la shilingi trilioni 2.45 kwa wakati, ili mfuko uweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi," alisema.

Madeni ya hatifungani NSSF, trilioni 1.39

Katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kamati hiyo imelieleza Bunge kuwa, mfuko huo unakumbana na changamoto za kutokamilika kwa mchakato wa kubadili madeni ya serikali na kuwa hati fungani ya muda maalumu (non-cash bond).

Kwa mujibu wa Tawfiq, jambo hilo linaathiri mapato ya uwekezaji wa mfuko kwa kiasi kikubwa, ambapo hadi kufikia Juni 2023, deni linalotokana na mikopo iliyotolewa na mfuko kugharamia miradi ya serikali lilifikia sh. trilioni 1.39, ambazo zinajumuisha sh. bilioni 624.33, ambazo ni mkopo halisi na riba ya sh. bilioni 769.58.

Kwenye madeni ya muda mrefu ya mifuko ya hifadhi ya jamii ya PSSSF na NSSF; Bunge limeazimia, serikali iandae mpango unaotekelezeka wa kulipa madeni ya mifuko ya hifadhi za jamii, ambayo ni mikopo ya miradi ya serikali na michango ya wanachama kwa upande wa PSSSF.

Katika suala la NSSF, serikali ichukue hatua kali za kisheria kwa waajiri wadanganyifu wanaowasilisha michango iliyo chini ya mshahara halisi wa mtumishi, kutotoa mikataba ya ajira na kuandikisha wanachama wachache kuliko waajiriwa walionao.

Kadhalika, NSSF iongeze kasi ya kuandikisha wanachama wapya ikiwa ni pamoja na kurejesha fao la matibabu kwa wanachama wa sekta isiyo rasmi, kwa lengo la kuvutia kundi hilo la wanachama.

# Aliyetoroka mahabusu polisi akamatwa baada ya siku 189

## -Ni anayedaiwa kunajisi mwanawe kwa miaka 3

Na Halfani Chusi

DANIEL Simle, aliyeripotiwa kutoroka Agosti Mosi, mwaka jana akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mvumi, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma, amekamatwa baada ya kusakwa na polisi kwa siku 189.

Mkazi huyo wa kijijini Ilewelo, kata ya Manzase, wilayani Chamwino, anadaiwa kufanya ukatili huo tangu mwaka 2021 dhidi ya mwanawe mwenye umri wa miaka tisa. Alikamatwa na polisi Julai 30, mwaka jana na kuwekwa mahabusu katika kituo hicho cha polisi, lakini jeshi hilo likadai alitoroka siku mbili baadaye.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Tabata, David Mwakinyuke amethibitisha kumshikilia mtuhumiwa huyo aliyefikishwa kituoni huko juzi saa tano usiku.

"Niseme kitu kimoja, ni kweli mtuhumiwa tunaye, kesi haijafunguliwa hapa kwetu. Mimi sina kitu chochote cha kusema, sisi utaratibu wetu hapa kwa sasa ni kuwasiliana na Polisi Dodoma ili waje kumchukua mtuhumiwa wao.

"Tunachokifanya hapa tumewapa taarifa. Watakuja kumchukua lini? Hilo si suala langu, lakini ninadhani haitachukua muda mrefu kwa sababu jambo hili linafahamika na watu wengi.

"Ni kweli jana tumempokea hapa mtuhumiwa na uzuri ni kwamba suala hilo nilikuwa ninalifahamu. Ningekuwa silifahamu ingebidi usiku huohuo nipate uhakika kutoka Dodoma ndio maana tulimpokea hapa na yuko mahabusu mpaka sasa," alisema Mwakinyuke ofisini kwake juzi alipozungumza na mwandishi wa habari hizi.

Mwakinyuke alipongeza mama wa mtoto huyo kulisaidia Jeshi la Polisi kumnasa mtuhumiwa huyo.

"Mkuu wa Upelelezi wa mwanzo kwa bahati mbaya amehamishwa, niliwasiliana naye, ndiye alinitumia hadi jina la polisi ambaye alifanya huo uzembe," alisema Mwakinyuke na kubainisha taratibu za kisheria wanazozingatia kumpeleka Dodoma mtuhumiwa huyo.

Mkuu wa Kituo huyo alisema atahakikisha mtuhumiwa huyo anakabidhiwa kwa Jeshi la Polisi mkoani Dodoma. Akiwatoroka tena, ni suala lililo nje ya mikono yake.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno.

### ALIVYOKAMATWA

Namna mtuhumiwa huyo alivyokamatwa, Shabani Abdalah, mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Tembomgwaza, Tabata, alimwambia mwandishi kuwa walikuwa na taarifa za tukio hilo walizopewa na mama wa mtoto ambaye ni mkazi wa eneo lake la uongozi.

Alibainisha kuwa baada ya mtuhumiwa kuripotiwa kuwatoroka polisi, walianza kupata fununu kupitia mama wa mtoto kuwa ameanza kuonekana katika maeneo ya Tabata walikoishi pamoja kabla ya kutengana. Na yeye kwenda kuishi Dodoma na mwanawe anayedaiwa kumfanyia ukatili huo Wakategа mitego.

"Siku za mwizi ni arobaini! Juzi tulipigiwa simu mtuhumiwa yupo kwenye mtaa wangu. Nilikuwa mbali, nikawaarifu sungusungu wa eneo langu washirikiane, wawahi eneo la tukio wamkamate.

"Ninamshukuru Mungu kwa kushirikiana na raia wema walimkamata mtuhumiwa. Waliniambia alitaka kukimbia lakini kwa kuwa walikuwa wamejipanga na walitawanyika sehemu nyingi, hakufanikiwa.

"Alikuwa tayari ameshamwandaa mwendeshaji bodaboda ili kukitokea lolote, wachomoke kwa urahisi, lakini walimwahi kabla hajapanda pikipiki," alidai.

Jonathan Mwasela, mmoja wa sungusungu waliomkamata Simle, alidai kuwa walipopata taarifa toka kwa mjumbe wao, walijipanga vizuri wakitambua kuwa walikuwa wanakwenda kukabiliana na mtuhumiwa ambaye ana rekodi ya kutoroka akiwa mahabusu ya polisi. Pia tuhuma zinazomkabili, zikithibitika adhabu yake ni kubwa - kifungo cha maisha gerezani.

"Alipotuona akahisi kama hatuna nia njema, akaanza kukimbia. Tukamwambia 'tutakuitia mwizi, simama'. Akasimama na watu walikuwa wamejaa tayari.

"Baada ya hapo tulimpeleka Kituo cha Polisi Tabata, walitupokea vizuri maana tunashirikiana vizuri sana na Jeshi la Polisi, hasa kwenye masuala haya yanayogusa maslahi ya jamii.

Sukaina (jina la pili tunalo), mama wa mtoto aliyefanyiwa ukatili huo, alimwambia mwandishi kuwa alijifanya hana tatizo na mumewe huyo wa zamani ili iwe rahisi kumvuta akamatwe.

Alisema kuwa baada ya mtuhumiwa kutoroka akiwa mahabusu ya polisi Agosti mwaka jana huku Jeshi la Polisi likiahidi kuhakikisha linamkamata tena, aliamua kusubiri hatua hiyo.

"Cha ajabu ilipofika mwezi wa 11 (Novemba) mwaka jana mtuhumiwa mwenyewe alinitafuta akiwa anataka kujua hali ya mtoto wake, nikamwambia 'anaendelea vizuri'.

"Siku hiyo aliponipigia simu, aliomba kuongea na mtoto, nikampa simu akaongea naye. Baadaye akasema 'nitakuja kuwasalimia', nikamwambia 'sawa'.

"Siku mbili baadaye, akanipigia simu, akiniarifu kwamba anakuja. Nikaenda kumweleza Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, tukaweka mtego pamoja na sungusungu, lakini hakutokea.

"Basi, baada ya hapo, jana (Jumatatu) akanipigia tena simu, akisema 'ninakuja, nipo njiani, nimewanunulia na watoto matikiti na ndizi'. Nikamwambia 'sawa, karibu sana na mimi nimekumisi sana mume wangu'," alisimulia mama huyo huku akihamia kwenye kilio kwa dakika kadhaa kisha anaendelea na masimulizi.

Alidai kuwa alimwambia mtuhumiwa kuwa akifika maeneo ya Tabata Kisukulu, ampigie simu ili aende kumpokea, huku akimlainisha kwa "maneno matamu", kumhakikishia bado anampenda licha ya ukatili anaodaiwa kufanya dhidi ya mwanawe. Kuhakikisha mtuhumiwa huyo anatiwa mbaroni, Sukaina alisema kuwa alitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ili waandae mtego. Ilipotimu saa tatu usiku ndipo alikamatwa na sungusungu na kufikishwa Kituo cha Polisi Tabata.

Sukaina alisema kuwa baada ya mtuhumiwa kufikishwa polisi, askari wa kituo hicho walimtaka afike kituoni huko akiwa na mwanawe asubuhi ya siku iliyofuata, yaani juzi kwa ajili ya taratibu zingine za kisheria.

Aliomba serikali imsaidie kesi yake isikilizwe na apatiwe haki yake kwa kuwa ametumia nguvu kubwa kuhakikisha mtuhumiwa anakamatwa tena, akiwa na ufafanuzi kuwa hana uwezo kiuchumi kusafiri kwenda Dodoma kutoa ushahidi kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa.

"Ninaumia sana, ninaiomba serikali iniangalie. Ninapaza sauti kwa Mama Samia, mimi ni mwanamke mwenzake, na aliyefanyiwa ukatili ni kama mjukuu wake, ni taifa la kesho. Kesi iende mahakamani ili haki ikapatikane huko, iwe fundisho na kwa wengine," alilalama Sukaina.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Tembomgwaza, Tabata, Veronica Mselle, alikokamatwa mtuhumiwa huyo, alithibitisha kupewa taarifa za ukatili huo na mama wa mtoto, wakaweka mtego uliofanikisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 131(3) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, mtu yeyote atakayetenda kosa la kubaka msichana wa chini ya umri wa miaka 10, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha gerezani.

Septemba 2-3, mwaka jana, Nipashe iliripoti kuhusu mtuhumiwa huyo kudaiwa na Jeshi la Polisi mkoani Dodoma kwamba alitoroka katika mahabusu ya Kituo cha Polisi Mvumi, wilayani Chamwino Agosti Mosi, mwaka jana, alikokuwa anashikiliwa kwa tuhuma za kunajisi mwanawe.

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### BEI MPYA ZA STEMPU ZA KODI ZA KIELEKTRONIKI (ETS)

**Dar es Salaam, 5 Februari, 2024:**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (2) ya Kanuni za stempu za kodi za kielektroniki za mwaka 2018, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) anapenda kuwatangazia bei mpya za stempu hizo kufuatia majadiliano yenye mafanikio makubwa kati ya Mamlaka ya Mapatao Tanzania (TRA), Umoja wa wenye viwanda Nchini Tanzania (CTI) na mkandarasi SICPA SA. Watengenezaji, Wazalishaji na Waagizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa na ambazo zimeorodheshwa katika jedwali la kwanza la kanuni za kodi za kielektroniki za mwaka 2018 watanunua stempu hizo kutoka kwa muuzaji aliyeingia mkataba na TRA kwa bei zilizoorodheshwa hapo chini.

Bei hizi mpya zimeanza kutumika kuanzia tarehe **24 Januari, 2024**. Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi ya TRA iliyopo karibu nawe au tembelea tovuti ya TRA **www.tra.go.tz** au piga simu bure kwenda namba **0800-780078** au **0800-750075** au **0800-110016,** WhatsApp **0744-233 333** au Barua pepe **services@tra.go.tz.**

| Na. | Aina ya Bidhaa | Chanzo | Bei ya zamani kwa '1000' | Bei Mpya kwa '1000' |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pombe kali, na pombe kali za mvuke | zote | 42,214.37 | 33,392.00 |
| | Mvinyo wa zabibu n.k | zote | 42,214.37 | 33,392.00 |
| 2 | Mvinyo wa matunda kama vile ndizi na nyanya n.k | Wenye matunda ya ndani kwa asilimia 75% au zaidi | 17,435.37 | 11,482.00 |
| | Sigara au bidhaa mbadala wa tumbaku | zote | 42,214.37 | 29,854.00 |
| 3 | Bidhaa nyingine za tumbaku n.k | zote | 42,214.37 | 29,854.00 |
| | Bia n.k | Zinazozalishwa nchini | 18,312.91 | 14,857.00 |
| 4 | Bia iliyotengenezwa kwa kimea n.k | Zinazoingizwa kutoka nje | 23,093.20 | 17,795.00 |
| | Juisi za matunda na mbogamboga | Zinazozalishwa nchini (kwa matunda ya ndani) | 8,082.62 | 6,889.00 |
| 5 | Juisi ya matunda ikiwemo ya zabibu, juisi ya mbogamboga zisizowekwa chachu. | Zinazoingizwa kutoka nje | 15,264.51 | 10,068.00 |
| 6 | Maji ya chupa | zote | 8,082.62 | 6,889.00 |
| | Vinywaji laini au maji yaliyoongezwa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujumuisha juisi za matunda. | Zilizo chini ya Tariff namba. 2202.10.00 | 8,082.62 | 6,889.00 |
| 7 | Vinywaji laini au maji yaliyoongezwa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujumuisha juisi za matunda. | Vinywaji vingine chini ya tariff namba 2202.91.00 na 2202.99.00 | 15,264.81 | 10,068.00 |
| 8 | Bidhaa za filamu na muziki (Yaani CD/VCDs/dvd/kanda zilizorekodiwa | zote | 16,165.24 | 16,165.24 |

Imetolewa na;

A.J.Kidata

**Kamishna Mkuu**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isikie kilio kuhusu utitiri mifuko uwezeshaji

**SERIKALI** katika awamu ya nne, iliibua sera na mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kuwasaidia Watanzania wengi ambao wanaishi katika umaskini uliotopea kuwa na hali bora ya maisha.

Suala hilo lilikuwamo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 kuhusu maisha bora kwa kila Mtanzania, lengo likiwa kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuanzisha miradi ya uzalishaji ambayo pamoja na kuinua uchumi wa mtu mmoja, familia, ingechangia pato la taifa kwa ujumla.

Baada ya kuingia madarakani kwa awamu hiyo chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, ulianzishwa mfuko chini ya iliyokuwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana uliokuwa unatoa fedha, maarufu kama 'Mabilioni ya Kikwete'. Hata hivyo, kutokana na usimamizi usioridhisha, mpango huo haukustawi na ulifutwa bila taarifa huku fedha zilizotolewa kwa wanufaika zikiishia hewani.

Baada ya hapo, liliimarishwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC) chini ya Tume ya Mipango ambalo linaendelea kutekeleza majukumu yake mpaka sasa na kuna mafanikio makubwa yanayoonekana mpaka sasa.

Pamoja na NEEC, kuna mifuko mingine mingi ambayo imekuwa ikijihusisha na uwezeshaji wananchi kiuchumi hali ambayo imesababisha mkanganyiko kutokana na kuwa chini ya wizara na idara tofauti za serikali. Hatua hiyo inasababisha kuwapo kwa ugumu wa uratibu na hata matokeo yake kutokuonekana kwa urahisi.

Aidha, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ambao bajeti yake haijatolewa kwa takribani miaka mitano, hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana. Pia kuna Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, ambayo inatishiwa na ufinyu wa bajeti.

Kutokana na kuwapo kwa utitiri huo na kuwapo shaka kuhusu ufanisi na kukosa tija, Bunge limeibuka na kutoa maazimio ya kuiagiza serikali kufanya tathmini ya haraka itakayoiongoza kuiunganisha na kuwa mfuko mmoja au michache itakayofanya kazi na kuleta matokeo chanya.

Akiwasilisha jana Bungeni, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu shughuli za kamati kwa mwaka 2023, Mwenyekiti wake, Fatma Tawfiq, alisema kutokana na wingi huo wa mifuko ya uwezeshaji wananchi, kamati inaona imekosa ufanisi, hivyo kushindwa kufikia tija iliyokusudiwa.


Kuwapo kwa wasiwasi huo kuhusu ufanisi, alisema kamati inaiagiza serikali ama kuwa na mfuko mmoja wenye nguvu au kuwa na michache ambayo itafanya kazi kwa ufanisi na hatimaye matokeo mazuri katika uwezeshaji wananchi na maendeleo endelevu kiuchumi kuonekana. Licha ya kufanya hivyo, kamati pia imeiagiza serikali kutoa fedha kwenye mifuko kama ilivyoainishwa katika bajeti ili itekeleze majukumu kwa ufanisi.

Azimio lililowekwa na bunge kuhusu utitiri wa mifuko hiyo unadhihirisha uhalisia kwamba nia ya serikali ni nzuri katika uwezeshaji wananchi kiuchumi lakini kwa hali ya sasa ni ngumu kuyaona matokeo. Kwa mantiki hiyo, ni vyema serikali ikasikia kilio cha bunge kupitia kamati ya maendeleo ya jamii ili kutekeleza maazimio na hatimaye kuwapo kwa ufanisi wa mifuko.

Kwa mtazamo yakinifu, NEEC inatosha kutekeleza jukumu hilo la uwezeshaji wananchi kiuchumi na lipewe nguvu na mamlaka katika kufanya kazi yake. Kwa upande wa bajeti, itengewe fungu la kutosha ambalo litawezesha wananchi kupata uwezo na kuanzisha miradi ya uzalishaji kama itakavyoona inafaa.

Vilevile, kama itawezekana, fedha zinazotolewa kwa ajili ya uwezeshaji huo kiuchumi isiwe katika mfumo wa ruzuku bali mikopo nafuu ili zizunguke na kuwafanya watu wengine kunufaika. Hatua hiyo ni dhahiri itakuwa na matokeo chanya na Watanzania wengi watanufaika na Uchumi wa nchi kukua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Darasa la WHO dhidi ya kansa na namna ilivyo vita kwa hatua

Na Tuntule Swebe

**MWEZI** huu wa pili kumefanyika Maadhimisho ya Siku ya Kansa Duniani Ilikuwa tarehe 4 hivyo, sisi kama jamii inatupasa tukumbuke, tulivyopoteza wapendwa wetu kwa ugonjwa huu kwani jamii nyingi duniani zimepoteza wapendwa wao ikiwamo wazazi, dada zao, kaka zao na hata wengine waka kosa haki zao za msingi baada ya kupoteza wazazi kwa ugonjwa huo

Inatupasa tusimame na tuangalie wapi tunatakiwa kurekebisha, pale panapowezekana, kwani inawezekana watu wetu wa karibu wanakufa kwa ugonjwa huo, kwa sababu ya kutokuwa na elimu juu ya hii, hivyo inatakiwa kujua mana ya kansa na chanzo chake, ili kuweza kuishi kwa tahadhari kuhusu ugonjwa huo

Saratani inasababishwa na chembe hai za mwili wa binadamu ambazo zinazaliana na kufa kwa mpangilio maalumu.

Chembe hizo zinapobadilika na kuzaliana bila ya utaratibu maalum, ndipo kunatokea maradhi ya saratani au kansa. Kuna aina za saratani ambazo mtu anaweza kupata; saratani ya shingo ya kizazi, saratani ya mapato , ugonjwa unaotegemea chembe.

Chembe zitapokimbilia mahali hapo, ndipo mgonjwa atapokuwa na ugonjwa huo mahali hapo, kuna visababishi vya ugonjwa huo ambavyo watu tunatakiwa tuchukue tahadhari zake.

Ugonjwa huo visababishi vyale vinaweza kuepukika, mfano ni uvutaji sigara au kutumia bidhaa za, tumbaku, mionzi ya jua na moshi. Ni hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa takwimu ya wagonjwa wanaofikiwa na vifo husika.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akatoa wito kwa Watanzania kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa saratani, kwa kuwa kila mwaka wagonjwa wanagundulika 40,000 na kuna vifo 26,000, hivyo Watanzania wasipochukua tahadhari vifo vitokanavyo na ugonjwa huo vitaongezeka.

Waziri Ummy ameshatamka kwenye Kikao cha Uwekezaji na Wadau wa Maendeleo kwa ajili ya uanzishwaji kituo cha umahiri cha matibabu ya saratani nchini kilichofunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kilichofanyika Jijini Dar Es Salaam.

"Wagonjwa wanaofika Hospitali ni asilimia 30 tu, wengi wapo mitaani na wanashindwa kufika katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya, tunawaasa Watanzania kufika katika vituo hivyo na kupata matibabu ya saratani, ili tupunguze wagonjwa pamoja na vifo" Waziri Ummy anatamka.

Anafafanua, kupitia mradi huo wa unaonzisha Kituo cha Huduma za Saratani nchini, kutasaidia kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi na muda wa matibabu kwa Wagonjwa.

"Nikiangalia takwimu zetu kwa mwaka 2021/22 wagonjwa 89 waliopelekwa nje ya nchi tumetumia shilingi bilioni 4.8 na kwa wagonjwa saratani pekee imetumika shilingi bilioni 3.1.

"Pia, kufuatia kituo hiki tutaongeza huduma za tiba utalii (Wagonjwa kutoka nje kuja kutibiwa Tanzania" anasema.

Akifafanua zaidi ya asilimia 80 ya wagonjwa wa saratani wanaofika hospitalini, hali zao zinakuwa katika hatua ya tatu hadi ya nne.

"Hali ambayo inapelekea kupata ugumu wa matibabu tofauti na ambavyo angewahi kujua hali yake na kuanza matibabu mapema.

"Nitoe wito kwa Watanzania wapime saratani angalau mara moja kwa mwaka, kwa kuwa saratani inayoongoza ni ya mlango wa kizazi kwa asilimia 25, matiti asilimia 10, tezi dume asilimia 9, mfumo wa chakula asilimia 6.5 na saratani nyinginezo," anasema Ummy

Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO), linafafanua asilimia 50 ya saratani zinazuilika, tamko lililotolewa kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kansa Duniani, tarehe 4 nwezi huu.

Pia, mwaka juzi ilitamkwa saratani nyingi zinaweza kuharibika na matokeo yake yakawa mazuri. Wito kwa watu wote msisahau kuwa kila mtoto anatakiwa kupata chanjo ya hepatasis B, ili kutokomeza ugonjwa huo, kwani ugonjwa huo hatari kijamii, ikipaswa kuepukwa.

Hapo inatajwa vitu visivyo na ulazima kama matumizi ya tumbaku, sigara na kutembea juani muda mrefu pasipo sababu za msingi, kwa pamoja tukiamua kuitokomeza kansa au saratani tunaweza.

Sababu ni kwamba, kama taifa bora na imara,yenye uthubutu wa kupambana na magonjwa yanayoweza kuzuilika. Mtu anapohisi maumivu kupita kiasi mahali popote pale ni vema ukamuona daktari.

HABARI KITAIFA

# Msichana asimulia alivyomwomba Rais cherehani moja akapewa tano

**Na Restuta James**

NI simulizi ya kusisimua ya msichana mwenye miaka 28, ambaye ni yatima asiyewafahamu baba na mama, aliyepewa msaada wa vyerehani na Rais Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni.

Si mwingine bali ni Beatrice Mwalingo, ambaye ujumbe wake wa maneno 10 umefanikisha kumtambulisha Rais Samia kwenye dunia ya ushonaji, wateja na kuongeza ajira kwa vijana.

Historia ya msichana huyo imebebwa kwa kiasi kikubwa na mageuzi ya teknolojia, kuanzia kujifunza kwake kushona hadi kukutana na msaada wa Rais Samia.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Beatrice anasema baba yake alikuwa Msafwa wa Mbeya akifanya biashara mpakani Tunduma na mama yake alikuwa askari polisi mpakani hapo wakati wanakutana.

"Sina baba wala mama. Nimelelewa na babu na bibi yangu mzaa mama. Bibi alishafariki, babu ndiye yupo na mimi ninamlea. Babu yuko Kigoma. Baba yangu simfahamu maana alifariki (dunia) nikiwa bado mdogo na mama alifariki (dunia) nikiwa na miaka minne," anasimulia.

Beatrice anasema kutokana na kuwapo kwa picha za mama yake, kunampa taswira fulani za maisha ya utoto akiwa naye lakini si kumbukumbu kamili.

"Mama alikuwa mtu wa kushinda kazini. Naweza kusema kupitia picha kumbukumbu inakuja," anasema.

**HISTORIA YA USHONAJI**

Kwa mujibu wa Beatrice, mitandao ya kijamii imebeba historia ya pekee katika kazi anayoifanya kwani alijifunza kushona kupitia mtandao wa Youtube.

"Nimejifunza kushona kupitia 'youtube' nikiwa Japan mwaka 2019. Nilinunua kicherehani kidogo nikawa nafanya mazoezi mpaka nilipoweza na kuamua kununua cherehani kubwa ambayo nilianza kuwashonea rafiki zangu," anasema.

Bila kueleza kwa undani, anasema alikwenda Japan akiishi na mpenzi wake aliyekuwa nchini humo. Kwa mwaka mmoja, anasema alifanya mazoezi kwa vitendo akiangalia youtube huku akijishonea nguo yeye na rafiki zake.

"Nina miaka mitano sasa tangu nianze kushonea rafiki zangu na baadhi ya wateja nikiwa kule kule Japan. Niliona naweza kufanya kitu kingine zaidi, nikapata wazo kwamba nikija Tanzania naweza kujiajiri na kuajiri mafundi ili nishone kwa wingi zaidi, ndipo mwaka jana nikafungua hii ofisi," anasema Beatrice.

Anasema ofisi hiyo ambayo iko eneo la Bomba Mbili, Kivule, Ilala jijini Dar es Salaam aliifungua Novemba, mwaka jana, akiwa na mafundi 12 ambao watano walikwenda kula sikukuu Desemba, mwaka jana, na hawajarejea.

Kuhusu kumtumia Rais ujumbe, anasema hakutarajia kujibiwa.

"Unajua watu wakiangalia page (ukurasa) ya Rais kila mmoja ana kitu chake cha kuandika. Sasa sijui mimi ni kwa vile nimezungukwa na cherehani kila siku ndilo wazo lililokuja la kuomba cherehani, lakini sikutarajia kama itakuja wala kwamba ataiona na kunijibu," anabainisha.

Akizungumzia ndoto aliyo nayo kwenye biashara yake, Beatrice anasema anaiona mbali na kwamba hata alipofika, hakufikiria. Mbali na kushona, msichana huyo anafuga kuku na bata kwa ajili ya biashara.

Beatrice ambaye bado hajaolewa wala hana mtoto, anasema mwaka jana alianza na kuku 500 ambao amewauza na sasa wamebakia chini ya 40. Anasema anafuga pia bata bukini na mbwa wasio wa ulinzi.

Mbali na kushona nguo za wateja wanaofika ofisini kwake, anashona pia nguo za harusi, mabegi ya safari, pochi na nguo za kike na za kiume anazouza kwenye maduka.

Anatoa rai kwa vijana na wanawake kutumia mitandao ya kijamii kujielimisha na pia wasikate tamaa katika kazi wanazofanya.

"Hata kama anapenda kupika, kushona au chochote kile, inabidi afanye mazoezi zaidi ili aendelee kupata uzoefu kuliko kusubiri hadi uwe umekamilika," anasema.

**UJUMBE WA MANENO 10 KWA RAIS**

Ujumbe wa Beatrice kwenye ukurasa wa Rais Samia ulisomeka: "Ukiwa unarudi nyumbani naomba unileteе zawadi ya cherehani" ambao ulijibiwa na Rais: "Hujambo Beatrice, nimepata wasaa wa kusoma ujumbe wako. Hongera kwa kazi na kujituma. Wasaidizi wangu watawasiliana na wewe kukusaidia upate mashine uliyoomba kwa shughuli zako. Nakutakia kila la kheri.'

**SIKU YA MAKABIDHIANO**

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kukabidhiwa cherehani nne kutoka kwa Rais Samia, Beatrice anasema zitamwongezea nguvu na ajira kwa vijana wanne. Beatrice alikabidhiwa cherehani nne ambazo ni mbili za kushona kawaida na mbili za kudarizi na hivyo kufanya awe na jumla ya vyerehani 14.

"Nimefurahi kwa sababu ni kitu ambacho sikukitarajia kwamba itakuja iwe ni kitu kikubwa zaidi na nilichokuwa natегеmea. Mimi nilivyoomba nilidhani nitapata moja, lakini namshukuru Mungu ameniagizia zaidi ya kile nilichoomba au nilichotarajia," anasema.

"Hii inaniongezea nguvu ya kuendelea kujituma zaidi na imenivusha kutoka hatua moja kwenda nyingine na kwa hili itawasaidia wenzangu zaidi. Kwa cherehani za kudarizi itanisaidia kwa sababu nitafanyia hapa hapa tofauti na mwanzo nilikuwa naenda kwa wenye nazo. Itakuwa urahisi wa kufanyakazi zaidi. Cherehani hizi zitaongeza ajira nne," anaongeza huku akibainisha kuwa alianza kwa kununua cherehani tano za mtumba na tano mpya.

"Nilivyopata meseji yake (Rais Samia) kwamba nitapata nilichokiomba imenifungulia milango mingine zaidi. Amenitambulisha kwa vijana wenzangu, wateja na kwa watu wengi sana, niseme tu ahsante sana kwake, najiona mwenye bahati," anasema na kwamba amepata wateja wengi na amefanikiwa kukutana na makundi mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari. "Natamani sana nimshonee nguo Mheshimiwa Rais na kama nitapata nafasi nimpime mwenyewe nimtengenezee nguo ila kwa leo nampa kuku watano kama zawadi kwakuwa nafuga pia," anasema.

Kuhusu matumizi ya mitandao kwa vijana, anasema: "Tusitumie mitandao kama sehemu ya kupunguzia hasira. Iwe ni sehemu ya kueleza changamoto au mahitaji yetu. Anaweza asikione mhusika wakapita watu wengine wakaguswa na wakakusaidia."



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kulia), akishauriana jambo na Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbolea ya ruzuku yatoroshwa mipaka ya Songwe na Kigoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amelieleza Bunge kuna wafanyabiashara wa mbolea wamekamatwa kwenye mipaka ya Songwe na Kigoma wakitorosha mbolea ya ruzuku.

Bashe alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina.

Mbunge huyo alisema usambazaji mbolea ya ruzuku kwa mwaka 2022/23 uligubikwa na changamoto nyingi ikiwamo wakulima kuuziwa mbolea feki, mbolea nyingi kutoroshwa na wakulima wengi kupata mbolea isiyotosheleza.

"Je, katika msimu huu 2023/24, serikali imejipanga vipi kutatua changamoto zilizojitokeza na kuleta hasara kwa wakulima?" Mpina alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Bashe alikiri kuwa ulipoanza mfumo wa ruzuku ya mbolea, kulikuwa na changamoto nyingi ikiwamo mfumo wa usambazaji na waagizaji mbolea kutokuwa waaminifu.

"Changamoto zilizokuwapo mwaka jana zimetatuliwa na serikali na tutaendelea kuboresha mfumo wa ruzuku, mwaka huu tumekumbana na changamoto ya baadhi ya wafanyabiashara kwenda kutafuta njia ya kutorosha mbolea kwa sababu wameshindwa kuiba kwenye mfumo, kuingiza takwimu za uongo," alisema.

Waziri Bashe alisema wamepata shida kwenye Mipaka ya Songwe na Kigoma ambako wamekamatwa wafanyabiashara na kufikishwa mahakamani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi.

"Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa ruzuku na hatutaacha mfumo wa ruzuku kwa sababu tunaamini tuna wajibu wa kusaidia wakulima wadogo na tutaendelea kukabiliana na changamoto zinazojitokeza," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, aliyehoji lini serikali itaweka utaratibu wa mbolea kuwekwa kwenye vifungashio vya ujazo huo.

Waziri Bashe, akijibu swali hilo, aliagiza wazalishaji na wasambazaji mbolea nchini kuanza kufungasha kwa ujazo kuanzia kilo tano, 10, 25 na 50 ili wakulima wamudu kununua kulingana na mahitaji yao.

Alisema serikali inatambua kuwa mahitaji ya mbolea kwa wakulima yanatofautiana hususan kwa wakulima wa mazao ya bustani na mazao mengine ya nafaka.

Alisema uhitaji wa mbolea kwa mazao ya bustani ni wa kiasi kidogo kulinganishwa na mazao mengine ikiwemo nafaka na mizizi.

Ili kukidhi mahitaji ya aina hiyo na matakwa ya Sheria na Kanuni ya 32(4) ya Kanuni za Mbolea za Mwaka 2011, Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) imeelekeza waingizaji, wazalishaji na wasambazaji mbolea nchini kuanza kufungasha mbolea katika ujazo unao tofautiana kuanzia kilo tano, 10, 25 na 50 ili kuwezesha wakulima kupata mbolea kulingana na mahitaji yao.

Alibainisha kuwa katika msimu wa 2023/24, kampuni tatu zimeshaanza kufungasha mbolea (ETG Inputs Limited, Yara Tanzania Limited na Minjingu Mines and Fertilizers Limited).

Alisema serikali inaendelea kuhimiza kampuni za mbolea nchini kufungasha katika ujazo tofauti ili kukidhi mahitaji ya wakulima, kuongeza matumizi ya mbolea na kupunguza vitendo vya baadhi ya mawakala kufungua mifuko.

Aliagiza kampuni zisibadili bei elekezi ambayo ni kilo 50 kuuzwa kwa Sh. 75,000, hivyo inatakiwa mifuko ya kilo moja isizidi kilo elekezi ya kilo 50 huku akiagiza TFRA wafuatilie popote zilipo kampuni hizo zinazofungasha ili kuhakikisha zinafuata mwongozo wa bei na pia watoe mwongozo wa kampuni hizo pia wafungashe kilo tano, 10, 20 na 50.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhiwa mzani na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji baada ya kuweka jiwe la msingi la ofisi za Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo (WMA), Medeli jijini Dodoma juzi. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa. **Habari Uk. 15. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bodi ya Tumbaku yatolea ufafanuzi madai kutumikisha watoto shambani

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

SIKU chache baada ya baadhi ya vyombo vya habari kuripoti madai kuwapo utumikishwaji watoto kwenye kilimo cha tumbaku, Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB) imelitolea ufafanuzi suala hilo.

Imesema kilimo cha zao hilo kinazingatia miongozo minne inayosimamia utekelezaji sheria ya ajira na ustawi wa jamii katika shughuli zinazohusiana na kilimo na biashara ya tumbaku nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa bodi hiyo, Stanley Mnozya, alitoa ufafanuzi huo mjini Kahama juzi alipozungumza na waandishi wa habari, akisema miongozo hiyo mikubwa kwa zao hilo inajumuisha utunzaji mazingira, utumikishwaji watoto, ubora wa tumbaku na malipo kwa wakulima.

Mnozya alisema sekta ya tumbaku ina sifa zake kidunia na si matakwa ya nchi. Ni biashara yenye maelekezo ya kuhakikisha watoto hawatumikishwi kwenye shughuli zozote zinazohusiana na kilimo cha tumbaku pamoja na kutokomeza ajira za watoto na aina nyingine za manyanyaso kwa wafanyakazi wanaojihusisha na uzalishaji zao hilo.

"Kwa mjibu wa kifungu namba 69 cha Kanuni za Sheria ya Tasnia ya Tumbaku za Mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2011, lengo la mwongozo huo ni kuweka mazingira mazuri na salama na ya haki katika mashamba yote ya tumbaku ili iweze kuendelea kuuzika kwa wateja wao wa soko la ndani na la nje ya nchi," alisema Stanley Mnozya.

Mwongozo huo umejegwa katika katika misingi ya viwango vya ajira vya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004, Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu Kanuni na Haki za Msingi Kazini pamoja na masharti mengine duniani ya shirika hilo la kimataifa.

Kauli ya mkurugenzi huyo imekuja baada ya kuibuka madai katika eneo la wakulima wa tumbaku Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama kwamba kilimo hicho kinafanyika kwa kukiuka miongozo hiyo, hivyo wahusika kwenda kinyume cha taratibu kisheria.

Mnozya alisema kwa kilimo cha Tanzania kwenye zao la tumbaku, wadau wote ikiwamo serikali, kampuni za ununuzi, vyama vya msingi na wakulima wenyewe wako makini kwenye kusimamia miongozo hiyo likiwamo zuio la utumikishwaji watoto.

Akizungumzia suala la utumikiswaji watoto kutoka nchi jirani za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mnozya alisema taratibu za kiuhamiaji zipo na zinafuatwa kwa mjibu wa sheria, hivyo hakuna mhamiaji anayeweza kuingia Tanzania akafanya kazi bila utaratibu.

Mmoja wa wakulima wakubwa wa tumbaku, Emmauel Shibuga anayemiliki maeneo mashamba katika eneo la Ushetu, yakiwamo yaliyoko Kata ya Ulowa, alisema ana zaidi ya miaka 20 anafanya kilimo cha tumbaku, hajakumbana na changamoto ya utumikishwaji watoto na raia wa kigeni .

Shibuga pia alisema hakuna tatizo lolote katika makubaliano kati ya wakulima na wafanyakazi katika mashamba ya tumbaku. Malipo yao baada ya msimu kumalizika huzingatiwa kwa kuwalipa stahiki zao zote na wakati wa kilimo mfanyakazi anapopata matatizo ya kuugua, mkulima huchukua gharama zote za matibabu bila kumkata mfanyakazi kwenye malipo yake.

Saimon Makaji ni mmoja wa wafanyakazi katika mashamba ya tumbaku wilayani Kahama. Alisema kazi hizo hufanywa na wanaume kwa kuwa nyingi zinahitaji kutumia nguvu na hakuna vibarua wa kike wanaofanya kazi za msimu za zao hilo.

Alisema kuwa huwa wanakubaliana na waajiri wao ambao ni wamiliki wa mashamba kuwapatia huduma zote ikiwamo chakula, malazi na matunzo mpaka wanapomaliza msimu na kuwalipa ujira wao.

Mratibu wa Mradi wa Kilimo na Mafunzo kwenye Kilimo cha Tumbaku kutoka Kampuni ya Ununuzi wa Tumbaku ya Mkwawa, Safari Laurent alisema wao kama wasimamizi, wanapita kila shamba kutoa mafunzo ya usimamizi wa mwongozo wa kilimo cha tumbaku kuhakikisha unazingatiwa na wanafanya ukaguzi wa wafanyakazi wote kuona kama wanakidhi umri. Hata kama mzazi wake ndiye mmilikiwa shamba, mtoto huyo haruhusiwi kushiriki shughuli za kilimo cha tumbaku.

Awali, Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Kahama, Salum Rashid Salum, alisema zipo taratibu za kisheria za kuingiza wahamiaji nchini kufanya kazi za vibarua vya msimu ambazo hufanywa na anayehitaji kwa kupatiwa kibali maalum.

Akizungumza na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Kahama (KACU) wakati, akitoa salamu za Jeshi la Uhamiaji, Salum alitaka wakulima wa zao hilo wanaohitaji vibarua katka mashamba yao, wafike ofisini kwake wapewe taratibu za kupata vibali.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema kilimo cha tumbaku wilayani mwake kinazingatia sheria za kimataifa zinazosimamia sekta hiyo na ndio maana Kahama sasa hivi ni ya pili kwa uzalishaji zao hilo nchini.

Alisema serikali iko makini kwa kila idara yake kuhakikisha miongozo yote ya kusimamia zao hilo inafuatwa.

# Kituo maalum cha matibabu ya saratani kujengwa mkoani Dodoma

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA na Marekani zimeingia makubaliano ya ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Saratani (TRACE) mkoani Dodoma kupitia mradi wa wawekezaji wa afya wa dunia (GHC).

Mradi huo utatekelezwa na Serikali ya Tanzania na sekta binafsi kwa kushirikiana na GHC, kikitarajiwa kutoa huduma pia Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Makubaliano hayo yalitiwa saini juzi jijini Dar es Salaam, mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na viongozi wengine, wakiwamo Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh.

Rais Dk. Mwinyi, akizungumzia mradi huo, alisema serikali inachukua hatua kwa kuweka miundombinu ya kinga na tiba ili kukabiliana na maradhi hayo.

"Kuna haja kuwekeza na kuhakikisha matibabu bora ya saratani kwa wagonjwa nchini na Afrika. Kila mmoja awe mahiri, mhamasishaji wa mabadiliko ambaye anaguswa na wengine wanaokabiliwa na changamoto hii.

"Ninawashukuru GHC katika kukabiliana na saratani. Ninashukuru pia wawekezaji wa ndani TPSF, CEO Roundtable na wote kuhakikisha huduma za saratani zinakuwa imara nchini," alisema.

Rais Dk. Mwinyi pia alishukuru Serikali ya Marekani na Rais wa Marekani, Joe Biden kwa kuhakikisha matibabu ya saratani yanaimarika nchini.

Naye Ummy alisema ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kusaidia utoaji huduma nchini na nchi jirani.

"Tunatarajia kupata Dola milioni moja kutoka sekta binafsi nchini, tutawafikia wadau wengine ili kuhakikisha tunakuwa na kituo bora cha saratani. Ninaishukuru GHC pamoja na Lancet kwa kuhamasisha kupata huduma bora.

"Miaka sita kutoka sasa vifo vitaongezeka. Sasa vifo ni 500,000 kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na tunaambiwa hadi kufika 2030 vitafikia 1,000,000.

"Nchini wagonjwa wapya ni takribani 40,000 vifo ni 26,000 kila mwaka. Wanaofika hospitalini kwa mwaka ni asilimia 30 tu. Wengi wapo majumbani kutokana na sababu tofauti.

"Mwaka 2018 mashine ya saratani ilifungwa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), zinatakwa kutibu wagonjwa 30 na sasa zinazidiwa kwa kutibu wagonjwa 70 kwa siku. Hata miaka yake ya uhai wa mashine hii unapungua na ninaambiwa inaanza kupungua ufanisi.

"Kwa miaka miwili tumeona wagonjwa wa saratani wapatao 124 kutoka nchi jirani, walifika kutibiwa nchini, kukamilika kwa kituo hiki kutaongeza utalii wa tiba," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo, alisema Tanzania ina uhaba wa madaktari bingwa wa saratani. Inakadiriwa kutakuwa na ongezeko la wagonjwa wa saratani duniani kutoka 500,000 hadi 1,000,000 ifikapo Mwaka 2030.

"Kuna upungufu wa madaktari bingwa wa saratani nchini, wapo 50 ni sawa na kusema bingwa mmoja anahudumia watu milioni moja. Kituo hiki kitapunguza foleni wa kusubiri radiotherapia kutoka miezi miwili hadi wiki moja," alisema Prof. Ruggajo.

Awali, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, alisema kutiwa saini kwa makubaliano hayo kunatokana na mkutano aliohudhuria Rais Samia Suluhu Hassan kati ya Afrika na Marekani.

Mkurugenzi wa taasisi ya Lancet, Prof. Wil Ngwa kutoka Marekani alisema matarajio ni kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na saratani kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2050.



# Taasisi za umma zaagizwa kujiunga eGA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi,Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameziagiza taasisi za umma kujiunga mifumo bora ya Serikali Mtandao (eGA) ili kuharakisha utoaji huduma kwa wananchi.

Waziri Simbachawene alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati akifungua kikao kazi cha nne cha eGA .

Vilevile, aliagiza taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutupiwa jicho la karibu kwa kuwa nyingi zilizoko pembezoni mwa nchi hazijajiunga na mfumo huo.

“Taasisi za umma kujiunga na mfumo huu ni lazima na siyo hiyari ili kuharakisha utoaji wa huduma kwa haraka wananchi.

“Hapa napenda kupongeza Idara ya Mahakama imepiga hatua kubwa katika eneo hilo. Lakini zipo taasisi za umma zinaingia katika mfumo kwa kulega lega hawa wanaita kwa sababu zao, sasa ni lazima taasisi zote kuhakikisha zinajiunga na mfumo huu,” alisema. Kuhusu serikali za mitaa, alisema serikali inapoteza mapato mengi kutokana na kutokuwa na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ukiwemo wa Tausi, mahususi kwa kufanya malipo pamoja na kuchelewesha kutoa huduma kwa wananchi. “Fedha nyingi za serikalini zinakaa kwenye mikono ya watu kwa muda mrefu bila sababu na hii inatokana na baadhi ya taasisi za umma, zikiwemo hamashauri kutotumia mfumo wa TEHAMA na kuhuisha kwa wakati,” alisema.

Simbachawene, alisema serikali inapenda kuona kila taasisi ya umma inaweka mkakati wa kuhakikisha mifumo yote ya mtandao inabadilisha taarifa zake na ili kufanikisha hilo, ni lazima zijiunge.

Vilevile aliagiza kuanzia kikao kazi cha mwaka ujao, wanatoa tuzo kwa washindi wa mfumo huo wa TEHAMA ili kuleta ushindani zaidi katika utendaji kazi.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Katibu Mkuu, Juma Mkoni, Tanzania ni miongoni mwa nchi ukanda wa jangwa la Sahara inaongoza kwa matumizi ya eGA.

Katibu Mkuu, Juma Mkoni, alisema kikao hicho kimehudhuriwa na wadau kutoka mashirika na taasisi za umma, wakiwemo maofisa masuuli, wakurugenzi na wakuu wa vitengo vya TEHAMA na watumiaji wengine wa mifumo ya teknolojia hiyo.

“Mwaka jana tulifanya kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao na kuweka maazimio 12, katika kikao hiki tutawasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo ni wakati mzuri kwa washiriki kufahamu yale waliyokubaliana na kutekeleza,” alisema

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele, alisema wizara yake inasimamia jukumu la kutunza ulinzi na usalama wa wananchi na kutoa huduma bora kwa jamii bila ubaguzi kwa kutumia TEHAMA.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya eGA, Dk. Jasmine Kusekwa, alizitaka taasisi za umma kutekeleza maagizo ya matumizi ya TEHAMA kwa kuwa ni takwa la kisheria.

Kaulimbiu ya kikao hicho kwa mwaka huu ni ‘Kuhakikisha uzingatiwaji wa sera, sheria viwango na miongozo ya serikali mtandao, kwa ubadilishaji salama wa taarifa’.



Polisi Kata ya Magila, wilayani Muheza mkoani Tanga, Frank Mwemsi akitoa elimu ya ulinzi shirikishi kwa wananchi, wakati wa mkutano wa hadhara katika kitongoji cha Kwegole, kijiji cha Mikwamba wilayani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vijiji jimbo la Muheza kupata maji bwelele

**Na Steven William,** MUHEZA

ADHA ya ukosefu maji kwa vijiji vilivyopo katika Jimbo la Muheza mkoani Tanga itakuwa historia baada ya baadhi kuanza kupata huduma hiyo kwa uhakika.

Ni baada ya wakazi wa Kijiji cha Kilulu kata ya Kilulu jimboni humo kusambaziwa maji hadi kwenye makazi yao baada ya mfadhili wa Taasisi ya Moo Maji Well Drilling Limited, Mohammed Ainahdi kuwachimbia kisima.

Taasisi hiyo imechimba kisima hicho na vingine takriban 79 katika vijiji mbalimbali jimboni humo.

Akizungumza na wananchi katika mkutano uliofanyika kiwanja cha stendi ya Bombani, Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo na Mbunge wa Muheza Hamisi Mwinjuma, aliishukuru taasisi hiyo kwa kukubali ombi lake na kuondoa malalamiko ya wakazi hao ya kukosa maji.

Alisema taasisi hiyo pia imeondoa adha kwenye nyumba za ibada, vituo vya afya, zahanati na shuleni kwa kujenga visima.

“Huyu mfadhili amekuwa mkombozi kwenye jimbo langu, amechimba visima vingine na kupeleka maji shule za sekondari na msingi, na kilichonisukuma kumtafuta tena ni upendo kwa wananchi wangu, ” alisema.

Alisema vilevile amepata visima 10 kutoka kwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kwa ajili ya kukabiliana na ukosefu wa maji kwa wakazi wa jimbo lake.

Alisema kwa sasa wanasubiri ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Pangani utakaogharimu Shilingi bilioni 40.

Alisema mkandarasi ameanza kupeleka mabomba kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo, ambao utaanza wakati wowote.

Awali Ainahdi, alisema amechimba visima hivyo katika jimbo hilo baada ya mbunge huyo kuwasilisha maombi juu ya uhitaji wa maji katika vijiji hivyo na kuwaondolea adha wananchi ya kukosa huduma hiyo.

“Mipango yetu ni kuendelea kusaidia kuchimba visima virefu katika vijiji, nyumba za ibada, shule za sekondari, msingi na hospitali na kuyasambaza kwa kutumia mabomba ya maji kutoka kwenye matangi makubwa, alisema.

# Wanaochafua viongozi CCM waonywa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANACHAMA wa Chama cha Mapinduzi (CCM), wameonywa kuacha siasa chafu kwa lengo la kuwachafua viongozi waliopo madarakani kwa kuwa chama hicho kitaendelea kuwalinda viongozi hao.

Onyo hilo limetolewa na Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI) na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Rabia Abdallah Hamid wakati wa Maadhimisho ya Miaka 47 ya kuzaliwa kwa kwa chama hicho yaliyofanyika Kata ya Kindi Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Alisema muda wa kufanya kampeni haujafika, hivyo CCM inatambua ina wabunge na madiwani na kuwataka wanachama wenye nia ya kugombea nafasi hizo kusubiri muda utakapofika. “Sisi tunawatambua viongozi ambao bado wako madarakani na tutawalinda ili watimize wajibu wao na kutekeleza Ilani ya CCM, “ alisema na kusisitiza kuwa:

“Wabunge na madiwani hawana shida ila shida inaletewa na watu wenye uchu wa madaraka ambao wamekuwa wakifanya siasa za kuwachafua, niwaonye wanachama wenye nia hiyo waache.”

Aliwataka wanachama wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kujengea tabia ya kuingia katika mitandao ya kijamii na kueleza kazi nzuri zinazofanywa na serikali.

“UVCCM mmefanikiwa katika maeneo mengi, lakini kwa mitandao ya kijamii mmejisahau na kuacha propaganda chafu kutapakaa, sasa ni wajibu wenu kuingia na kujibu kwa kuonyesha ukweli,” alisema Rabia.

Kwa upande mwingine, aliwakumbusha viongozi wa CCM na serikali kuendelea kusimamia fedha zinazoletwa na Serikali kwa Mkoa wa Kilimanjaro ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mwenyekiti wa CCM wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, alisema tangu kuasisiwa kwa kwa chama hicho, kimefanya mambo mkoani humo kwa maslahi ya wananchi na kuwataka wanachama kutembea kifua mbele na kujivunia mafanikio hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kwa kipindi cha miaka miwili na nusu, wamepokea Shilingi bilioni 821 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Babu, alisema serikali itaendelea kuhakikisha matatizo yanayowakabili wananchi yanapatiwa ufumbuzi.



# Wanafunzi Mriba wasota chini

**Na Timothy Itembe,** MARA

WANAFUNZI wa kidato cha kwanza na cha pili katika Shule ya Sekondari ya Mriba ya Halmashauri ya Tarime Vijijini mkoani hapa wanakaa chini kutokana na uhaba wa madawati.

Kero hiyo imeibuliwa juzi na Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Waitara aliishauri halmashuri hiyo kutumia fedha zilizotengwa kutengeneza madawati kwa shule za msingi na sekondari na kuwaondolea kero wanafunzi ya kukaa chini.

Waitara, alishauri fedha hizo zitumike kuwalipa mafundi wa kutengeneza madawati na mbao zivunwe kutoka msitu iliyopo kwenye halmashauri hiyo ili kupunguza ukubwa wa bajeti.

Kutokana na hali hiyo, madiwani walipendekeza fedha za madawati 6,059 zaidi ya Shilingi milioni 510 na Shilingi milioni 349 kwa ajili ya seti ya viti zilizotengwa zitumike kuwaondolea adha wanafunzi hao ya kukaa chini.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Diwani wa Kata ya Regicheri, Johnbosko Mbusiro, alishauri fedha zilizotengwa za uwajibikaji kwa jamii kutoka mgodi wa North Mara Gold Mine kununulia madawati, zitumike kutengeneza madawati kwa shule za msingi na sekondari za halmashauri hiyo.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Solomon Shati, alisema bajeti iliyotengwa haitakidhi utengenezaji wa madawati kwa shule hizo, licha ya fedha hizo kuonekana kuwa nyingi.

Shati, aliwataka madiwani kubuni mbinu ya kumaliza adha hiyo.



Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Fungo (kushoto), akizungumza na walimu wakuu wa shule za msingi na wakuu wa sekondari, wakati akiwahamasisha kuongeza ufaulu wa wanafunzi wao mashuleni, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Sh. 5,000 yakwamisha wanafunzi kuripoti shule

**Na Rose Jacob,** UKEREWE

WAKAZI wilayani hapa Mkoa wa Mwanza wamedai tozo ya shilingi 5,000 kupima afya imechangia wanafunzi wengi kuchelewa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kutokana na wazazi kushindwa kulipa kwa kukosa fedha.

Wakizungumza na Nipashe nje ya Kikao cha Baraza Madiwani cha kujadili bajeti ya halmashauri ya Ukerewe kwa mwaka 2024/2025, walisema huduma ya upimaji afya kwa wanafunzi iendelee kutolewa bure kwa wanaojiunga na sekondari.

Waliomba huduma hiyo iondolewe kwa wanafunzi wanaojiunga na shule ya msingi kama ilivyokuwa awali ili kuwarahisishia wazazi kuwapeleka watoto wao shule.

"Ukimpeleka mtoto kupima daktari anachukua fomu anaijaza na kugonga mhuri bila kumpima, sasa sisi wazazi tunabaki kujiuliza kinachotakiwa ni Shilingi 5,000, lakini afya ya mtoto siyo kitu, hivyo tunaiomba serikali iliangalie hili," alisema Kazimili Majula, Mkazi wa Mansion. Diwani wa Kata ya Nyamanga iliyoko Tarafa ya Ukara, Mussa Malima alisema, ulipaji wa Shilingi 5,000 ya upimaji wa afya kwa wanafunzi unaleta adha kubwa kwa wananchi wengi kutokana na kipato duni.

"Mkuu wa Wilaya alifanya ziara ya kutembelea shule za kata mbalimbali, ikiwemo tarafa yetu ambako katika Shule ya Sekondari Bukungu alikuta wanafunzi walio ripoti ni watatu kati ya 220 na shule ya Nyamanga saba kati ya zaidi ya 100 sababu ni kupima afya tu," alisema Malima.

Alisema ingawa wapo wazazi wanaopeleka watoto wao kupima afya, watumishi wa sekta hiyo wasiowaaminifu wamekuwa wakipokea fomu hizo na kuzijaza bila kumpima mwanafunzi na fedha kuweka mfukoni.

Alisema hali hiyo inakwamisha lengo la kukusanya mapato ya halmashauri kwani fedha haziingii kwenye mfumo husika na badala yake kwenye mifuko ya watu binafsi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Joshua Manumbu akihitimisha kikao hicho, alisema upimaji afya kwa mwanafunzi ni kwa mujibu wa sheria ya uchangiaji wa huduma za afya.

Manumbu, alisema halmashauri hiyo ya Ukerewe ilipitisha sheria ndogo mwaka 2018 inayoelekeza upimaji wa afya katika kada mbalimbali ikwemo wanafunzi,wahudumu wa baa na hoteli na mamalishe.

"Kutokana na kuonekana upimaji wa afya kwa gharama ya Shilingi 5,000 kuwa ni kero kwa wazazi, hasa kwakuzingatia Rais Samia Suluhu Hassan amebeba majukumu mengi ya elimu bure, madiwani waliomba hii tozo iondolewe, kanuni zinavyoelekeza huwezi kuiondoa bila utaratibu kufuatwa," alisema na kuongeza kuwa:

"Baraza tumekubaliana tuiache Shilingi 5,000 ya upimaji afya kwa wanafunzi iendelee hadi tutakapokuwa kwenye vikao vya robo tutaanzisha mchakato wa uboreshaji sheria ndogo ndogo hizi."

# Mvua na jua vyawaibua wadau wa mazingira

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WADAU wa mazingira mkoani hapa wameanzisha kampeni ya upandaji wa miti zaidi ya 1,000 katika maeneo ya wazi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuhimiza usafi wa mazingira.

Wadau hao wa ni pamoja na Wanafunzi wa Chuo cha Mtakatifu Augustine Tanzania (SAUT) na Idara ya Mawasiliano ya Umma wabobevu katika Mahusiano kwa umma (PR) wakiwashirikisha askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Mwanza Transit Camp (MCT) na Shirika lisilo la kiserikari la Synergistic Globe.

Akizungumza jana wakati wa upandaji miti 500 katika eneo la wazi, Mratibu wa kampeni hiyo ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Synergistic Globe, Mhadhiri Angelina Tabu Manyama, alisema hatua hiyo imekuja baada ya kubaini kuwa mvua za kupitiliza zimekuwa zikinyesha na jua lisilo la wastani kuwaka.

Alisema hali hiyo inatokana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea kutokea duniani kutokana na uharibifu wa mazingira, uchomaji na ukataji miti ovyo, matumizi ya kuni, uchafuzi wa plastiki na uzalishaji wa hewa ya kaboni. "Hali hii siyo ya kuikalia kimya ndiyo maana tumeanza kwa kupanda miti 500 na shughuli hii ni endelevu, tutapanda miti mingi zaidi katika maeneo ya uhifadhi wa mazingira eneo la Ziwa Victoria," alisema Manyama.

Mkuu wa Idara cha Mawasiliano ya Umma, Dk. Peter Mataba, alisema jukumu la utunzaji wa mazingira ni la kila Mtanzania, hivyo ni vyema wanafunzi wakajikita bada ya kujifunza darasani na kuwa mabalozi katika jamii zao. "Tunaheshimu juhudi zenye mashiko za kuhakikisha Tanzania inakuwa ni ya kijani, kampeni hii inakuwa endelevu kwani lengo letu ni kupanda miti 1,000," alisema Dk. Mataba.

Mwakilishi wa Synergistic Globe, Silivanus Mashishi, alisema ushiriki wao katika upandaji miti ni sehemu ya kuhimiza jamii kuhifadhi, kutunza mazingira na vyanzo vya maji katika maeneo yao kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

# ama

ALHAMISI FEBRUARI 8, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Mlipuko wa mimba utotoni makambi wakimbizi UNFPA, Japan waungana



Ukurasa 12

## Hospitali Bugando katika mapinduzi ya tiba vichwa vikubwa, mgongo wazi

### MMAM & SAFARI YA 2030 SDGS...

# Rais anavyopambana na Wizara Afya tija wodini, kupunguza vifo

## • Mwanza, Arusha watangaza nuru vituo afya

**Na Christina Mwakangale**

AKIANGALIWA kwa kina, kisiasa na hata kiutawala, sekta zote zinazohusika na malezi ya jamii, daima Rais Dk, Samia Suluhu Hasssan, amedumu yuko makini na mkali hasa.

Hapo inajumuisha Wizara ya Afya, ambako tangu aingie madarakani amewateua kinamama kama yeye kuiongoza waweze kuilea.

Kimataifa, pia ndio wizara iliyoachiwa jukumu la kutumikia Lengo Namba Tatu la Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), ikilenga afya na ustawi bora kwa jamii.


Hadi sasa, historia ya kupokezana kijiti cha uongozi kitaifa ikiwamo kuendeleza Mpango wa Maendekeo ya Afya ya Msingi (AMA) iliyoanza mwaka 2008, uwekezaji katika sekta afya bajeti yake imekua maradufu kutoka Sh. bilioni 845 mwaka 2016/2017 hadi shilingi trilioni 1.2 mwaka 2023/2024.

Zao lake la moja kwa moja, ni Rais Dk. Samia anendeleza katika zama zake, kwamba vifo vitokanavyo na uzazi nchini vimepungua kutoka 530 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022. Ni punguzo la asilimia 80.37.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Mwka 2022 (TDHS-MIS), miongoni mwa vipaumbele vya serikali ya Rais Samia, ni kufikia malengo ya SDGs 2030.

Akizindua ripori TDHS-MIS anasema, Rais Dk. Samia anasema: "Kiwango kimepungua kwa asilimia 80, Mwenyezi Mungu atuwezeshe tuendelee.

"Shabaha ya Malengo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030 inaelekeza kupunguza vifo vya mama wakati wa uzazi na visizidi 70 kwa kila vizazi hai 100,000, sasa hivi tuko 104, safari yetu mpaka mwaka 2030 tunaweza kufikia hii shabaha."



Watoa huduma za afya katika chumba maalum cha kuhudumia watoto wachanga (ICU), katika Hospitali ya Rufani Mount Meru, mjini Arusha wakiwa kazini. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE.**

**KUTOKA UN**

Akihudhuria kikao cha Umoja wa Mataifa kinachohusu afya, Septemba mwaka jana, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akimwakilisha Rais Dk. Samia, akawahakikishi kikaoni namna Serikali ya Tanzania imejidhatiti kutekeleza malengo ya kufikisha huduma za afya kwa wote hadi ifikapo mwaka 2030.

Kilikuwa kikao cha Huduma za Afya kwa wote kilichofanyika kwenye Mkutano Mkuu wa 78 wa Umoja wa Mataifa, jijini New York, Marekani, Septemba mwaka jana.

Ummy akafafanua "Tanzania inaungana na wajumbe wengine wa kikao hiki katika kutekeleza azimio hili la kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa huduma bora za afya popote alipo."

Anasema, upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi nchini imeendelea kuimarika kutoka asilimia 38 mwaka 2015 hadi asilimia 43 mwaka 2022, huku bajeti ya afya ikiendelea kuboreshwa maradufu kutoka Dola Milioni 529 (Sh. bilioni 1.343) mwaka 2019 hadi kufikia Dola Milioni 950 (Sh. bilioni 2.413) mwaka 2022, Dk. Samia akiwa na mwaka mmoa ofisini.

Waziri Ummy anasema Tanzania imeendelea kutekeleza Azimio la Afya kwa Wote waliloweka viongozi wakuu wa nchi kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 2019, ikilenga kuboresha upatikanaji huduma za afya kwa wote, kuhamasisha wananchi kujiunga na skimu za bima ya afya.

"Serikali ya Tanzania inaendelea kutenga fedha kuhakikisha inafikia lengo la afya kwa wote, ikiwamo kuwasilisha muswada wa Bima ya afya kwa Wote katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". Akatamka Waziri Ummy. Muswada huo ulishawalishwa bungeni.

Waziri Ummy katika kikaoa hicho jijini New York, Marekani, akaeleza kufikia lengo la afya kwa wote ni lazima huduma za afya ngazi ya msingi ziboreshwe, ili wananchi wazipate kwa karibu.

Pia, akataka haja ya kuimarishwa utoaji elimu ya afya na kuongeza nguvu za mapambano dhidi ya magonjwa na utoaji tiba. Kimsingi, ndio jukumu la AMA na mkazo wa serikali ya Awamu ya Sita.

"Tunahimiza ushirikiano wa pamoja kati ya serikali na wadau wa sekta ya afya kuungana pamoja katika kufikia malengo tuliyoweka ya afya kwa wote hadi ifikapo mwaka 2030,": anaisistzia akiwa na nyongeza:

"Kwa kuwekeza kwenye Ubunifu wa Teknolojia mpya, Rasilimali, mbinu bora za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza pamoja na huduma za chanjo na dawa."

**KULIVYO MWANZA/ARUSHA**

Mbali na Dar es Salaam, mikoa mingine yenye maeneo ya hadhi ya jiji ni Mwanza, Mbeya na Arusha, hata kupafanya pawe na mahitaji makubwa ya huduma afya, penye jiji na nje ya hapo.

Nipashe, ilifanya ziara katika

**Inaendelea Uk. 13**

AFYA

# Hospitali Bugando katika mapinduzi ya tiba vichwa vikubwa, mgongo wazi

## •Shida wakitakiwa kurudi, 62% wanatokomea
## •Kila mwaka wapya 345, waendao kliniki 700

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

UGONJWA vichwa kujaa maji, pia mgongo wazi, zinatajwa janga kwa watoto, likihitaji huduma za udhibiti kusogezwa kwa wahitaji.

Hadi sasa kuna kilio wazazi hawana fedha kuwatibu.

Katika Hospitali ya Rufani Kanda, Bugando, jijini Mwanza penye huduma kwa kundi hilo, kumepokewa watoto 345 wapya wenye matatizo hayo mwaka jana.

Pia, wanaohudhuria kliniki ni takribani 700. huku asilimia 62 wanaofanyiwa upasuaji wanatoweka kutokana na kushindwa kumudu tiba.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo na Mgongo hospitalini hapo, Gerald Mayaya (pichani), anataja nusu ya waliofika kutibiwa wanatoka Kanda ya Ziwa na mikoa jirani kama Tabora, Manyara, Singida na Kigoma.

Dk. Gerald anaeleza umri wao ni chini ya miaka 13, huku watoto wanaowafanyia upasuaji, asilimia 38 pekee ndio hurejea kwa uangalizi zaidi. Hapo anataja sababu kuu ni uchumi, wakikosa nauli na fedha za kujikimu, wakati kunahitajika mtoto afike hospitalini mara tano hadi sita kwa mwaka, baada ya upasuaji.

"Fikiria mtoto yupo Bukoba, kusafiri mara tano hadi sita kufuata huduma unakuwa mtihani. Ukweli, watoto wengi hawafiki hospitalini na wanaotibiwa wengi hawarejei kufanyiwa uchunguzi na kuangalia maendeleo yao.

"Unaweza kumuwekea mpira, akifika huko unaziba na hawezi kurudi tena. Pia, wototo wengi wanachelewa kuja kwenye matibabu, mfano mtoto alipata shida akiwa na mwezi mmoja au kazaliwa nao, anakuja baada ya miezi sita.

"Baadaye hapo unakuta ubongo tayari umeathirika sana na akifanyiwa operesheni matokeo yanakuwa siyo mazuri sana," anaeleza Dk.Gerald.

**CHANZO KUJAA MAJI**

Dk. Gerald anaifafanulia Nipashe, kwamba kichwa kujaa maji kuliko kawaida, ni kwamba kila mwanadamu ana maji kwenye ubongo, ila shida ni pale yanapokuwa mengi kwenye ubongo, kuliko mahitaji.

Anafafanua wastani wa hayo maji ni milimita 500 kwa kila mwanadamu aliye sawa, ndani ya saa 24. Maji hayo yanapita kwenye mfumo wa damu na kinachobaki ni kwenye mzunguko; hiyo ni kati ya milimita 100 na 150. Inapotokea hitilafu, ndio tatizo hujitokeza.

Vilevile, anasema inawezekana ikawa anapozaliwa au baada ya kuzaliwa na nyiginezo nyingi. Kuwapo sehemu nyembamba inayopitisha maji kwenye ubongo, nayo inachangia maji kutopita vizuri.

"Kuna baadhi watoto wanaozaliwa wakiwa wachanga, kuna sehemu za ubongo zinavuja damu, wanaweza kupata shida hiyo," anasema Dk. Gerald.

Anasema, mara nyingi watoto wanaopata shida kichwa kujaa maji baada ya kuzaliwa, huanzia miezi mitatu hadi sita ya kwanza, ikichangiwa na maambukizi, ingawaje wachache wanaopata shida hiyo baada ya miezi sita.



**VYANZO VYAKE**

Mtaalamu huyo anataja chanzo cha kichwa kikubwa kuongezeka, ni mifupa inayozunguka ubongo mtoto anapozaliwa isipojiunga na maji yanapozidi kujaa, yanaisukuma mifupa, hata kuchangia kichwa kuwa kikubwa.

Bingwa huyo anaueleza mgongo wazi, umegawanyika sehemu mbili. Mosi, ni kwa baadhi ya watoto wanaozaliwa na uvimbe mgongoni, unaweza kuwa juu ya mgongo, chini ya mgongo, mpaka shingoni.

Pia, Dk. Gerald anataja shingoni au katikati ya mgongo kwa mtoto anayezaliwa kunakuwapo kasoro zinazogusa mifupa na mifumo ya fahamu.

Sehemu nyingine kwa watoto hawajazaliwa na uvimbe, mara nyingi siyo rahisi kugundua na baada ya kuwa watu wazima, miaka 20 hadi 30 au zaidi, ndio wanaanza kusikia maumivu mgongoni hadi miguuni na ganzi endelevu.

Hapo mtaalamu anafafanua, watoto hao wanapokaguliwa kiafya, kunakutwa na shimo mgongoni na kitabibu anapogundulika, anafanyiwa upasuaji haraka na ikiwezekana mara nyingi, wengi waanarudi sawa. Wapo wanaokutwa, choo na mkojo vinawatoka, huku miguu haina nguvu.

**NINI KIFANYIKE?**

Dk. Gerald, anataja kwa matatizo yote mawili mzazi anakingwa kwa kupatiwa vidonge 'folic acid' mfululizo miezi mitatu kabla ya ujauzito au ujauzito ukiwa na wiki moja.

Anaeleza mtu anapojigundua ana shida mgongo wazi kwa siku 20 hadi 28 za kwanza za ujauzito, anatumia dawa, vilevile inashauriwa atumie dawa miezi mitatu kabla, anopohisi anaweza kuwa mjamzito au mara baada ya tendo la ndoa.

Pia, kunatajwa mzazi wa mtoto mwenye shida hiyo, ana uwezekano mkubwa akapata mwingine aina hiyo, hivyo anakumbushwa kuweka dawa vituoni watoto, kunusuru maambukizi baada ya kuzaliwa .

Vipimo kwa watoto anavitaja ni 'ultrasound ya ubongo' inayowaonyesha hitilafu na kubaini vinginevyo, hata kuwapa njia bora kitabibu kama vile kufanyika upasuaji.

Pia, matibabu yamegawanyika katika sehemu tatu; Mosi mtu kuwekewa mpira kutoka kwenye ubongo kwenda tumboni, ikimuwezesha kuendelea na shughuli zake, akikaa na mipira hiyo maisha yote.

Njia nyingine ni kwa wagonjwa wenye uvimbe wa ubongo kwa asilimia 70, hufanyiwa upasuaji, Dk. Gerald akisema kuna watoto wanaofanyiwa upasuaji wakarejea hali kawaida, kutegemea alivyoathirika.

Hata hivyo, analalamika kuwapo watoto wananaopaswa kuhudhuria Bugando, baadhi ya maelekezo ya kitabibu, hawatimzi.

"Ukimwangalia mtoto unasema angewaishwa matokeo yangekuwa mazuri sana, kwa sababu ukimfanyia operesheni mapema, matokeo yanakuwa mazuri," anatamka na kuendelea;

"Anapomchelewesha, mara nyingi kuna baadhi wanakuwa na ulemavu wa kudumu, ikiwamo kutoweza kutembea na vifo vinaweza kutokea."

Mtalaamu anafafanua, kuwapo watoto wanaowekewa mpira kisha inaziba ndani ya mwezi mmoja, asiporudi hosptalini inamaanisha tatizo linajirudia, lakini akihudhria anabadilishiwa mpira.

Vilevile Dk. Gerald, anakumbusha asipopata matibabu, kichwa kinazidi kuwa kikubwa na baadhi vinapasuka .

**KWA WATU WAZIMA**

Mtaalamu huyo anaeleza mtu yeyote anaweza kupata tatizo hilo nakila mwezi, Bugando wanapata wagonjwa wenye shida wawili, dalili kuu ni huwa maumivu makali kichwani wanashindwa kulala au kushindwa kufanya chochote, hasa asubuhi, wanatapika, miguu inakosa nguvu kuna wakati wanapoteza fahamu .

Anasema watu wazima wanafanyiwa kipimo cha 'CT Scan' au 'MRI', kwa sababu kichwa chake kimeshafungamana na sehemu 'ultra sound' inaweza kupitishwa.

Anaeleza, watu wazima wanawawekewa mpira kutokana na shida yake, pia anafanyiwa upasuaji endapo kuna uvimbe kwenye ubongo.

Hapo kunatolewa uzoefu wa waliopata ajali za barabarani, ikachangia damu zao kuvilia kwenye njia ya maji, inasababisha maji kuziba na upasuaji unahitajika mara nyingi. Tiba yake anataja kukiwapo na majaribio baada ya mwaka mmoja, mhusika anaishi pasipo mpira.

"Mgonjwa wetu wa mwisho ambaye tulijaribu kuangalia uwezekano wa kuishi bila mpira alikuwa ni mgonjwa kutoka Kalemie nchini Congo (DRC). Alipata ajali huko Kalemie, wakamsafirisha hadi Mwanza.

"Tulimfanyia upasuaji mwaka jana, alikuwa hajitambui kabisa! Tulifanya upasuaji huo ndani ya siku tatu, baada ya muda akawa sawa, akaanza kutembea kama kawaida na tukamruhusu kuondoka.

"Baada ya mwaka mmoja tulihitaji kuona kama anaweza kuishi bila mpira ambao tulimtolea, lakini ndani ya masaa 24 tu kichwa kilimuuma sana na baada ya 'Ct Scan' tulibaini hawezi kuishi bila mpira. Tunawasiliana naye kila wakati na anaendelea vizuri," anaeleza

**WADAU TIBA.**

Walter Miya ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwanangu Development Tanzania, anaeleza wanashirikiana na hospitali kufadhili matibabu ya watoto hao, mwaka 2018 walianzisha nyumba ya matumaini kunusuru mrundikano wa watoto wodini.

Pia, anasema kuna watoto wanaotoka mbali na hawana ndugu Mwanza wanakotibiwa na wanahitajika kwa siku kadhaa, panakuwa msaada kwao.

Nipashe ikazumgumza na mzazi Rozy Kenedy, mama wa Watoto wanne, mkazi wa Magu mkoani Mwanza, akiwa na mtoto mwenye tatizo kichwa kinajaa maji kuliko kawaida, anakiri ushirikiano na elimu ya aliyoipata kwa madaktari wa Bugando, mwanaweza kafanyiwa upasuaji akiwa na umri siku 18, sasa anaendelea vizuri.

"Nilikuwa siwezi kuona sura ya binti yangu vizuri, kichwa kilikuwa kikubwa, lakini sasa hivi ukimwangalia huwezi kuamini, kimeanza kupungua na uzuri wa mwanangu umeanza kuonekana, namshukuru sana Dk.Gerald..." anatamka. Pia, Kulwa Isamalaja wa Sengerema, mwenye mtoto mgongo wazi, anaeleza jamii iache kutowajali watoto wa namna hiyo, huku akiwaomba baba zao wawape ushirikiano wa kina kuwasaidia watoto kwa shida zao

"Tunaiomba serikali itusogezee huduma (Sengerema), kuja huku ni gharama kutokana na hali duni ya kimaisha tunashindwa kuwapeleka watoto hospitali mapema, pia kuwepo mazingira mazuri ya kusomea watoto hao na kuwapatia walimu maalumu," anahitmisha.

AFYA

# Mlipuko wa mimba utotoni makambi wakimbizi UNFPA, Japan waungana

## • Mil. 921/- za Afya, Mama na Mtoto, Kigoma

**Na Sabato Kasika**

NI kwa wastani, kambi za wakimbizi Nyarugusu na Nduta wilayani Kasulu na Kibondo mkoani Kigoma, zinashuhudia takriban mimba za utotoni 2004 kila mwezi.

Mbali na kuwapo kwa idadi hiyo ya mimba, kila mwezi takriban wanawake 201 hukumbana na matatizo ya afya ya uzazi na mimba kuharibika.

Chanzo cha tatizo ni nini? Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner, anataja ni kukosekana elimu ya afya ya uzazi.

Schreiner anatamka hayo nyumbani kwa Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa, Dar es Salaam wiki iliyopita katika hafla ya kutia saini makubaliano ya kutekeleza, mradi huo kwa muda wa mwaka mmoja wa 2024, ambao Japan inadhamini Sh. milioni 921 ili kuutekeleza.

Anafafanua zaidi Mwakilishi Mkazi huyo, akisema, katika kipindi chote cha mwaka 2022 wote lake pamoja na washirika wake lilifanikiwa kuzuia vifo vya mama wajawazito, katika kambi hizo.

Washirika hao ni Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Borderless Tanzania Ltd na shirika la kikundi cha Borderless Japan Corporation.

"Kushirikiana na washirika tulisimamia huduma za afya ya uzazi ikiwamo kuelimisha umuhimu wa kuzingatia maelekezo ya wataalam wana - afya.



Balozi Yasushi Misawa (kulia) na Mark Bryan Schreiner wakitia saini hati ya makubaliano ya kuboresha Afya ya Mama na Mtoto, katuia makambi ya wakimbizi mkoani-Kigoma. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Katika chote cha mwaka huo, hakukuwa na kifo hata kimoja kinachotokea kwa mjamzito wakati wa kujifungua, ikiwa ni matunda ya juhudi za kuboresha afya ya mama na mtoto," anasema Schreiner.

Anasema, wakati huo kambi ya Nyarugusu ilikuwa na wakimbizi 136,478 huku Nduta, ikiwa na wakimbizi 64,010, na kwamba sasa wamekuja wapya waliongia tangu mwanzoni mwa mwaka uliopita. "Mazingira hayo yanatufanya turudi tena Kigoma kwa ajili ya kutekeleza mradi huo kwa mara nyingine, ili kuboresha afya ya uzazi, kwani kuna wakimbizi wapya 14, 540 kutoka Congo DR wanawake wakiwa asilimia 56," anasema.

Anafafanua kuwa wakimbizi hao wapya wamekuja wakati shirika hilo na tayari limeshaondoka, hali inayosababisha kuwapo idadi kubwa ya mimba hizo.

"Hivyo, ubalozi wa Japan nchini Tanzania na sisi UNFPA, tumetia saini makubaliano ya ufadhili shilingi milioni 921, ili kuokoa maisha wakimbizi na wakazi wa jirani na kambi hizo," anasema.

Schreiner anaeleza fedha hizo zitatumika kununua vifaa muhimu vya matibabu na kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya 50, wakiwamo madaktari 25 na wauguzi 25 ili kuboresha huduma ya uzazi.

Anafafanua, pia kupitia fedha hizo watanunua gari la kisasa litakalotumika kuratibu shughuli afya ya uzazi katika kambi hizo na maeneo ya jirani.

"Pia, wataajiriwa watumishi wa afya15, ili waweze kuhudumia wakimbizi na watu waishio karibu na kambi hizo," anasema, akitamka wanawake na mabinti wakimbizi 3,000, pia wakazi jirani 3,000 wa kambi hizo watapata taulo za kike kwa muda wa mwaka mmoja," anatamka.

Schreiner anasema, ni mradi utakaonufaisha zaidi ya watu 113,000, kuanzia wanawake, mabinti wakiwamo waliopata mimba za utotoni, wavulana wa umri balehe na wenye ulemavu waishio ndani na nje ya kambi za wakimbizi.

"Tunaishukuru Japan kwa kufadhili jitihada zetu hizi za kuokoa maisha ya wanawake na wasichana katika kambi za wakimbizi ambazo zinasimamiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," anasema.

**MFADHILI ANENA**

Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa anasema, Japan imejikita katika kuboresha afya kwa watu duniani kote ili kufikia lengo la maendeleo endelevu, lionalotaka watu wote duniani wanapata huduma ya afya.

"Japan inawekeza katika miradi inayoboresha maisha ya wanawake na kulinda wanawake na watoto walioathiriwa na migogoro na majanga ya asili," anasema Misawa.

Anafafanua kuwa Japan na Tanzania hadi sasa zinafurahia uhusiano wa kirafiki tangu uhuru wa nchi mwaka 1961, nchi ikisaidia maendeleo ya Tanzania kijamii na kiuchumi.

Balozi Misawa ana ufafanuzi kwamba ushirikiano wa nchi hizo mbili, unahusisha sekta mbalimbali, kuanzia kilimo, utawala bora, viwanda na maendeleo ya watu, na kwamba huduma ya afya ni mojawapo ya maeneo ya kipaumbele ya ushirikiano huo.

Pia, ninashukuru serikali ya Tanzania kwa juhudi zake kubwa za kuboresha huduma za afya. Uongozi wa Rais Samia (Suluhu Hassan), uko wazi kuhusu umuhimu wa kutoa huduma bora ya afya kwa maendeleo ya watu nchini," anasema.

Aidha, anaeleza namna Japan imejitolea kuboresha afya ya watu duniani kote na kwamba katika Mkutano wa Nane wa Kimataifa wa Tokyo wa Maendeleo ya Afrika (TICAD8), uliofanyika nchini Tunisia mwaka 2022, Waziri Mkuu wa Japan Kishida akasisitiza umuhimu wa sekta ya afya na kutangaza kuwa Japan itazingatia hilo.

# Rais anavyopambana na Wizara Afya kupunguza vifo...

**Inatoka Uk. 11**

mikoa hiyo kwa baadhi ya wilaya kama vile Ilemela, Magu mkoani Mwanza pamoja Meru, Arusha DC, ikibaini ujenzi wa majengo na maboresho ya huduma, ununuzi wa vifaa tiba, magari ya wagonjwa na yanayotoa tiba temebezi.

Aina hiyo ya maboresho, nyuma ya pazia imeimarishwa kutokana na sababu tofauti zinazotajwa na wakuu wa afya kwenye mikoa hiyo; kuna huduma zianzotokana na fedha kutoka serikali kuu, ikiwamo kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF) nchini.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Pima Sebastian anaeleza: "Utekelezaji wa fedha za Mfuko wa Pamoja yaani HBF kwa mwaka wa fedha uliopita 2021/2022 tulikuwa na shilingi milioni 687 na tukapokea asilimia asilimia 87 ya fedha hizo.

"Kati ya fedha hizo, ziko ambazo zilinunua dawa kwa ajili ya mama na mtoto, vitanda vya kujifungulia, vifaa vya vyumba vya upasuaji katika Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya Bulale.

"Tumepunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 98 mwaka 2022 hadi 81 mwaka 2023. Uboresjani wa miundombinu tumepokea Sh. mil 900 kwa mwaka wa fedha ulioisha (2023) ajili ya uboreshaji miundombinu."

Aidha, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Charles Mkombachepa, anajumuisha yaliyoko katika afya mkoani mwake, kipindi cha 2021/22 na 2022/23,a akisema vimeongezeka vituo vya upasuaji kutoka 17 hadi 22.

Hapo anaeleza, zimelenga kupunguza vifaa vya mama na mtoto na kwamba vifo vitokanavyo na uzazi wanaojifungua, vimepungua mkoani kutoka 61 mwaka 2021 hadi kufikia 39 mwaka 2023.

**WAGANGA WAFAWIDHI**

Waganga wafawidhi katika vituo vya afya kwenye mikoa hiyo, wameeleza namna huduma zilizvyoimarika, ukiongezeka ufanisi wa kazi ikiwamo kupunguza rufani kutoka kituo kimoja kwenda hospitali za mkoa, wilaya na hospitali za rufani.

Kadhalika, wanabainisha huduma hizo kuboresha kama vile ujenzi wa vyumba vya upasuaji wajawazito kumechangia kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Buzuruga wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza, Dk. William Ntinginya, anasema mwaka 2021/2022 uwezo wa kuhudumia wanaojifungua kwa mwezi ilikuwa 200 hadi 300 na sasa mwaka 2024 uwezo umefikia 600.

"Operesheni (upasuaji) kwa wanaojifungua zimeongezeka hadi 70 inafika hata 100 awali ilikuwa 20 mpaka 30 kwa mwezi. Kwa siku tuanaona wajawazito 90 hadi 150, hao ni wanaokuja kuanza huduma na wanaoendelea," anasema na kutolea ufafanuzi: "Vifo vya uzazi 2021/2022 vilikuwa vitatu na 2022/23 vilikuwa vinne."

Dk. Bijengo Mabiba, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kisesa, wilayani Magu mkoani Mwanza, anasema mazingira yao kufanyia kazi yameboreshwa.

"Awali hatukuwa na jengo la upasuaji na mjamzito ilipotakiwa afanyiwe upasuaji tulimpa rufani, hospitali ya Bugando. Idadi ya wanaojifungua ilikuwa 180 kwa mwezi, ila sasa wanafikia 300 hadi 350.

"Eneo hili liko barabarani hivyo kuna majeruhi wa ajali wengi, zamani ilikuwa unawahudumia wagonjwa wa OPD hapo hapo na wagonjwa wa dharura.

"Pia, zamani kinamama wakati wanajifungua ilikuwa hakuna kutenganishwa, mama anajifungua na jirani yake anamuangalia, sasa kila mama anajifungua katika sehemu yake," anasema Dk. Bijengo.

**KAULI YA WANUFAIKA**

Zakaria Mbise (74), ni mkazi wa kijiji cha Imbaseni, Kata ya Imbaseni, wilaya Meru mkoani Arusha, anasema kwa miaka mingi huduma zilipatikana mbali hadi pale wananchi walipoamua kujitolea.

"Mimi umri umekwenda, lakini nawaonea huruma wenye umri mdogo. Mzazi akihitaji usafiri kwenda kufuata huduma mbali zaidi ya kilomita 10. Imani yetu ipo kwa kuwa jengo hili likikamilika, wazee tutapata msaada hivi karibuni.

"Tunaomba serikali isaidie jengo hili likamilike na vifaa tiba viwepo na watoa huduma."

AFYA

## IMEGAWANYIKA KATIKA AINA 200...

# Pilipili; kiungo kitamu kilichozoeleka, thamani lishe tele ila...mlaji ajiandae

**Na Mwandishi Wetu**

IWE ni nyekundu, kijani kibichi, rangi ya chungwa au manjano, pilipili ni moja ya viungo vinavyotumika kila mahali, ladha yake inapendwa, kuwa na sifa za kiafya zisizotarajiwa na ambazo wataalamu wa lishe wanashauri, binadamu yeyote awe nazo.

Athari ya pilipili katika mchuzi, inafurahiwa na kuna wanaoamini ni muhimu kunywa pombe kiasi ili kukabiliana na chakula “ kilichoungwa vizuri.”

**TAFSIRI YA WATAALAMU**

Jina pilipili linalopewa mimea kutoka kwa familia ya ‘Solanaceae’, ambayo matunda yake hutumiwa kama kitoweo au mboga. Inajulikana kuwa kali.

Na kuna zaidi ya aina 200 za pilipili zilizowekwa katika aina tano kwa mujibu wa mtaalamu wa lishe, usafi na ubora wa chakula, Dk. Mathieu Tobossi, anayebainisha kuwa tofauti zinapatikana katika sura, rangi, nguvu ya viungo na ukubwa wa hii. viungo.

Inakumbushwa, kipengele cha ukali cha pilipili kinahusishwa na kuwapo kwa sehemu inayoitwa ‘capsaicin’ inayotoa nguvu hiyop kwa viungo.

Zipo pilipili ambazo ‘capsaicin’ iko kwenye kiwango cha sifuri (pilipili kwa mfano), kiwango moja (kaprika), kiwango cha pili hadi cha tano inaangukia katika pilipili kali.

Pia, kuna kiwango cha sita, pilipili kali ‘cayenne’; kiwango cha saba pilipili kali ‘arbol’; kiwango cha nane ‘pilipili ya ndege’; tisa pilipili ya ‘tabasco’; kiwango cha 10 pilipili inayolipuka ‘abanero’.

Ni tunda lenye virutubishi vingi na madini mengi na na hivyo kuifanya pilipili kuwa mshirika mkubwa katika lishe ya kupunguza uzito.

**SIFA ZA KITABIBU**

Mtaalamu wa lishe, hasa anazungumzia pilipili nyekundu (cayenne) ambayo ingekuwa na sifa nyingi zaidi.

Pilipili hasa ‘cayenne’ anaitaja kusaidia kupunguza maumivu na kuboresha utendaji wa wanariadha, kulingana na utafiti uliopofanyika. Ni viungo viavyosaidia kurekebisha na kudhibiti viwango vya sukari ya damu.



Pilipili hoho ikiwa shambani. **PICHA ZOTE; MAKTABA.**

“Vipengele hivyo vyote huruhusu pilipili ili kukuza kuchoma mafuta na kupunguza uchovu,” anasema Dk Tobossi, akiongeza pia ni kipengele kinachopigana kwa ufanisi dhidi ya matatizo anayoyaita ‘oxidative.’

Mtaalamu huyo anaitaja pilipili kuchochea hamu ya kula na inakuza mzunguko wa damu kwa sababu ya kuwapo ‘capsaicin.’

Inapendekezwa, watu wanaokabiliwa na uvimbe wa tumbo kutumia, pia inaondoa mvutano wa misuli na maumivu.

Kuhusu pilipili nyekundu (cayenne), mtaalamu wa lishe anaizungumzia kwa sifa nyingi zaidi, akitamka: “Ina nguvu ya kupunguza kwa kiasi kikubwa maumivu kutokana na ‘arthritis’, maumivu ya mishipa, shingo, tumbo na maumivu ya mgongo.

“Utafiti umeonyesha kuwa ulaji pilipili wa mara kwa mara, unahusishwa na kupunguza hatari ya kifo kutokana na ugonjwa wa moyo na mishipa,” anasisitiza.

Hata hivyo katika uhalisia, inatajwa wengi wanaamini kuwa pilipili ndio chanzo cha tatizo la vidonda vya tumbo.

Mtaalamu wa lishe anasisitiza zaidi kuwa, pilipili huimarisha afya ya matumbo kuhusiana na usafirishaji vyakula, hata hivyo akishauri mbao tayari wana vidonda waepuke kula pilipili kali, kwa sababu inaweza kuongeza maumivu kwenye tumbo.

Wataalamu wa chakula wanasema kwamba hakuna hatari katika kula pilipili, isipokuwa haipaswi kutumiwa vibaya kwa kiasi kikubwa, kwa sababu inaathiri ute wa utumbo.

Wataalamu hao wa lishe wanashauri wale ambao tayari wana vidonda waepuke kula pilipili, haswa kali, kwa sababu “inaweza kuongeza maumivu” tumboni

Ligine wanalosahuri kwa wale ambao tayari wana vidonda waepuke kula pilipili, kwa sababu “inaweza kuongeza maumivu” tumboni.

“Kiungo chochote cha viungo huwa na mwelekeo wa kuchochea vidonda,” anaonya Dk. Mathieu Tobossi, anayewashauri wenye vidonda kuwa waangalifu wanapokula pilipili.

Hii hasa inahusu pilipili kali yenye muwasho, ambayo inapaswa kuepukwa. Ushauri huo unahusu watu wanaougua magonjwa fulani mahususi ikiwa ni pamoja na: Tezi dume; mipasuko ya njia ya haja kubwa; tatizo la kemikali tumboni; maambukizi ya njia ya mkojo, ugonjwa wa utumbo; mzio kwa pilipili; na vidonda vya tumbo



Mkulima wa Manguajuki, Manispaa ya Singida, akikagua bidhaa yake ‘pilipili kichaa’.

**THAMANI YAKE**

Hapa, mtaalamu wa lishe anasisitiza pilipili aina ya , cayenne (pilipili nyekundu) inayotumiwa sana duniani kote, inaweza kufikia urefu wa sentimeta tatu hadi nne.

Muundo wa lishe wa pilipili ya ‘cayenne’ una asilimia 66 ya wanga na asilimia 20 ya ‘lipid ‘(aina ya mafuta yanayofanya kazi mbalimbali mwilini na asilimia 14 ni protini.

Anataja kwamba huota juu juu sana wa nishati mwilini ikiwa na kalori 321 na mafuta yake ‘lipids’ huyeyuka kirahisi na haziwezi kusababisha ‘cholesterol’ katika mishipa ya damu au moyo.

Mboga hiyo anaonyesha ina kalori chache, sukari kidogo na ina maji na nyuzi nyuzi zinazosaidia katika usagaji wa chakula.

Aidha anasema ina madini kama vile chuma, shaba, manganese, fosforasi na magnesiamu. “Tunapokula kiasi pilipili nyekundu kila siku tunapata lishe ya yenye vitamini A, C na B, ambao hupatikana ,” anaarifu Dk. Mathieu Tobossi.

Hapo kunashauriwa kuwapo maono mazuri na rangi ya kuangaza, Vitamini C inayosafisha mwili (antioxidant) kusaidiana na mifumo ya kinga na neva mwilini, zikifaidika na vitamini B6 iliyomo kwenye pilipili hiyo.

Pia, kunakuwapo kiungo cha vitamini K, kinachosaidia uimarishaji mifupa. Pia, kuna potasiamu ambayo husaidia kurekebisha shinikizo la damu na zinki, ambayo huchangia uponyaji wa jeraha.

Kuna viungo vya flavonoids na carotenoids kwenye pilipili hoho ambavyo “vinasaidia kupunguza madhara ya sumu za kikaboni kama vile na mkazo wa oksidi ambao hutuzeesha haraka,” anaongeza mtaalamu huyo wa lishe.

Ni darasa linalokuacha kusuka au kuonyoa, kutoka thamani lishe na madhara yatokanayo na mlo pilipili, ambao sifa yake kuu ni muwasho mbao ndio mada kuu ya utamu wenyewe.

**•Kwa mujibu wa BBC**





# Majaliwa awaagiza WMA kufanya operesheni kuondoa lumbesa

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza viongozi wa Wakala wa Vipimo (WMA) kukomesha matumizi ya kipimo cha lumbesa kinachotumika na wafanyabaishara kwenye bidhaa za mazao, ili kuwasaidia wakulima kunufaika na kilimo.

Alitoa agizo hilo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa jengo la makao makuu ya wakala huo.

Majaliwa alisema tatizo la lumbesa limekuwa la muda mrefu na wakulima nchini wamekuwa wakilalamika mara nyingi lakini bado linajirudia na kuendelea kuwatesa.

"Wakulima licha kutumia nguvu nyingi bado wanaumizwa kwenye kipimo cha lumbesa, hivyo basi wakala nendeni mkalifanyie kazi suala hili kama mtu anataka vitunguu kilo 100 basi apate kilo hizo na kifungashio kiwe cha ujazo huo siyo vinginevyo" alisema Majaliwa

Aidha, aliwataka wafanyabishara nchini kuzingatia vipimo na kuacha tabia ya kujinufaisha kwa kuwaibia wengine.

"Wafanyabiashara acheni kulegeza vipimo vilivyowekwa, acheni kuwaibia wengine na wananchi tunabidi kuwa wajanja kila tumapohitaji bidhaa lazima kuzingatia ujazo kwa mujibu wa vipimo vilivyowekwa kisheria" alisisitiza Majaliwa.

Kadhalika, aliwata watumishi wa WMA kusimamia vyema sheria pamoja kanuni zake na kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa vipimo mara kwa mara katika maeneo mbalimbali nchini.

Kuhusu ujenzi wa jengo hilo, aliwapongeza WMA kwa kutekeleza maagizo ya serikali ya taasisi zote za umma kuwa na ofisi makao makuu ya nchi.

"Nawapongeza kwa kutekeleza maagizo ya serikali ya kuwa na jengo makao makuu hapa Dodoma katika ujenzi huu mnapaswa kuzingatia thamani ya fedha.

"Lakini pia naziagiza taasisi nyingine kuhakikisha kuwa wanatekeleza maelekezo haya ili kuipunguzia mzigo serikali wa fedha kwa ajili ya kupanga nyumba za ofisi"alisema.

Akizungumzia ujenzi wa mji wa kiserikali Mtumba awamu ya pili alisema umefikia asilimia 73.4 kwa majengo yote 29 ambayo yanajengwa hivi sasa.

"Hadi kufikia Januari mwaka huu ujenzi wa majengo ya mji wa kiserikali awamu ya pili umefikia asilimia 73.4 lakini zipo wizara ambazo ujenzi wa majengo yake umefikia asilimia zaidi ya 90," alisema.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akitolea ufafanuzi kuhusu kipimo cha lumbesa alisema tayari serikali imeshaunda tume ambayo inafanyia kazi jambo hilo na itakuja na majibu namna bora ya kulimaliza.

"Hivi sasa ipo tume ambayo inafanyia kazi suala la lumbesa na itakuja na majibu ili kabla ya mwaka mpya wa fedha 2024/2025 kuanza serikali tutatoa maagizo kwa mujibu wa sheria ya fedha kuhusu lumbesa"alisema.

Akizungumza kuhusu ujenzi wa jengo hilo alisema limefikia asilimia 70.34 na tayari Sh. bilioni 3.25 zimeshalipwa kwa mkandarasi kati ya Sh. bilioni 6.73 zinazohitajika kukamilisha mradi huo.

Alisema: "Mheshimiwa Waziri Mkuu ujenzi huu unatekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani ya taasisi yetu na hadi sasa umeshatekelezwa kwa muda wa miezi 18 na ukimalizika utasaidia sana kuondoa tatizo la uhaba wa ofisi na kupunguza gharama za kupanga majengo binafsi".



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, Bungeni jijini Dodoma jana kuhusu maandalizi ya mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola unaotarajiwa kufanyika Machi 4-8 mwaka huu huko Unguja Zanzibar. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Utawala bora, amani, vyaibeba Tanzania kimataifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk.Pindi Chana ametaja vigezo vilivyoibeba Tanzania kupewa uenyeji wa mkutano wa mawaziri wanaosimamia sheria kwenye nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola kuwa ni hali ya utawala bora, amani na utulivu uliopo nchini.

Alitaja sifa hizo jana mkoani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo.

Alisema mkutano huo utahudhuriwa na wanachama wa jumuiya hiyo kutoka nchi 56 na utafanyika kuanzia Machi 4 hadi 8 mwaka huu.

Amesema katika mkutano huo Tanzania itawania tuzo mbili ambazo ni usajili wa watoto chini ya miaka mitano pamoja na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kupitia kampeni ya Mama Samia Legal Aid Campaign.

"Dhima ya mkutano huu ni teknolojia na ubunifu katika masuala ya sheria na Tanzania inawania tuzo mbalimbali zitakazokuwepo kwenye mkutano huo na maandalizi yanaendelea ya mkutano kwa njia mbalimbali, utahudhuriwa na wageni takriban 300 wa nchi hizo,"alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan atafungua mkutano huo Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kuhusu kampeni ya msaada wa kisheria, Dk.Pindi alisema tayari imezinduliwa kwenye mikoa sita ikiwamo Dodoma na lengo ni kutoa msaada wa kisheria bure kwa wananchi wenye shida ya masuala ya sheria.

"Haya yote anayoyafanya Rais ni utawala wa sheria na kigezo ambavyo vimetumika kuamua mkutano wa 10 uende wapi wanaangalia hivi nchi yenyewe kweli ina utawala wa sheria, wamengalia Tanzania mambo ni safi," alisema.

"Kwasasa tupo kidijitali katika mahakama zetu, mtu akisomewa hukumu inarekodi kama bunge tunakwenda kidijitali kuna maboresho mengi sana na ndio 4R za Rais,"alisema.

# RC atangaza utaratibu mpya kuwapima maofisa ugani

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amesema utaanza utaratibu wa kuwapima utendaji wa kazi maofisa ugani kwa vigezo vinne ambavyo kama watashindwa kuvitimiza ajira zao zitakuwa rehani.

Alisema hayo jana wakati wa kikao kazi cha kupokea taarifa ya hali ya usambazaji wa mbolea na mbegu za alizeti zenye ruzuku ya serikali katika halmashauri.

Kikao hicho kiliwashirikisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa kilimo, wawekezaji wenye viwanda, viongozi wa dini na taasisi mbalimbali za mkoani hapa.

"Ninawaagiza wakurugenzi wa halmashauri wawe wananipa ripoti ya maofisa ugani kila wilaya ambapo tumeweka vigezo vinne, kwamza, wametembelea wakulima wangapi, pili, matumizi ya mbolea, Je? amehamasisha wakulima wangapi kwenye eneo lake, tatu, ugawaji wa mbegu za alizeti na nne Je? amepima mashamba mangapi afya ya udongo," alisema.

Serukamba, alisema maofisa kilimo wanapaswaa kuweka mkazo katika kuwaelimisha wakulima umuhimu wa kutumia mbolea na mbegu bora kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ili mkoa uweze kuingia katika ramani ya uzalishaji nchini.

"Rais ametuletea pikipiki 195 Mkoa wa Singida na kila ofisa ugani ana pikipiki, hivyo hana sababu ya kutotembelea wakulima mnataka nini, naombeni nendeni mkatekeleze wajibu wenu," alisema Serukamba.

Alisema kama hakutakuwa na matumizi sahihi ya mbolea na mbegu bora Mkoa wa Singida tutabakia kusikiliza yanaingia sikio hili na kutoka sikio lingine na kilimo kinabaki kuwa kile kile.

"Kazi yenu maofisa kilimo ni kwenda kuongea na wakulima na kuwaambia kuna umuhimu wa kutumia mbolea, mbegu sahihi na kulima sawa sawa, kuhakikisha mnapima afya ya udongo ya kila mkulima ili mnamweleza shamba lako hili unatakiwa utumie mbolea kiasi hiki, tukifanya hivyo niwahakikishie Singida itaingia kwenye ramani ya uzalishaji wa nchi hii," alisema.

Pia alisema serikali inajitahidi kuwekeza kwenye kilimo katika Mkoa wa Singida ambapo inaleta mbegu za alizeti ambazo zinazozalishwa na Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA) zinaletwa Singida.

"Leo hii kuna zaidi ya miradi mikubwa ya umwagiliaji na mingine ipo njiani inakuja ambayo itagharimu zaidi ya Sh. bilioni 50, kama serikali inawekeza kiasi hiki katika mkoa wetu halafu maofisa kilimo hatuwasaidii wakulima wajue mbinu bora za kilimo umaskini unaondokaje," alihoji Serukamba.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema ili kuweza kubaini eneo gani kuna upungufu wa utoaji wa mbolea na mbegu, maofisa kilimo wafanye utafiti wa kila kijiji na kata na maeneo ambako pembejeo hizo hazijafika mikakati ya kupeleka ifanyike haraka.

Alisema: "Tukishabaini kijiji au kata fulani bado mbolea na mbegu haijafika Mwenyekiti wa Kijiji husika aitishe mkutano wa wananchi kuwaeleza mbolea na mbegu zinapopatikana".





# Waogopa kubeba ujauzito kisa huduma hafifu za afya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANAWAKE wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wamesema wanaogopa kubeba ujauzito wakihofia kupata matatizo ya kiafya, wakidai uwepo wa huduma hafifu za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wilayani humo.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela uliokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Mmoja wa wanawake hao, Maria Mwaikunga alisema wajawazito wamekuwa wakikaa muda mrefu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya bila kuhudumia hali ambayo inawasababishia usumbufu usiokuwa wa lazima.

Alisema wajawazito wanaweza wakaenda kwenye kituo cha afya kwa ajili ya kupata huduma lakini wanakaa mpaka jioni na huwa hawaelezwi sababu za kutohudumiwa kwa wakati.

"Kwa sasa tunaogopa hata kubeba mimba, tukienda na mimba zetu tunakaa mpaka jioni bila kuhudumiwa, kwahiyo tunaomba tusaidiwe hili jambo linatukera sana," alisema Maria.

Naye Canisia Sanga alisema wakati mwingine wanakwenda kwenye vituo va afya hasa zahanati kwa lengo la kupima maendeleo ya ujauzito lakini wanaambiwa vipimo havipo na kutakiwa kwenda kupima kwenye vituo vya watu binafsi.

Alisema wanawake wamekuwa wakikerwa na tatizo hilo la kukosekana kwa vipimo kwa maelezo kuwa vituo hivyo vinakuwa havina maana kwao kwa maelezo kuwa huwa wanaongezewa gharama ambazo hazina msingi wowote.

Aliiomba serikali kushughulikia tatizo hilo haraka ili kuwapunguzia wanawake tatizo hilo la kuhangaika kutafuta huduma muhimu za afya wanapokuwa wajawazito.

"Tunaishukuru sana serikali imejitahidi kutusogezea huduma za afya kwa kutujengea zahanati na vituo vya afya, sasa tunaomba pia mtusaidie kuondoa tatizo hili la kukosekana kwa vipimo," alisema Canisia.

Akijibu kero hiyo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Dk. Darison Andrew alisema tatizo la kukosekana kwa vipimo kwenye vituo vya afya kunatokana na kukwama kwa fedha za kununulia vifaa hivyo kwenye mfumo.

Alisema zaidi ya Sh. milioni 700 ambazo zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye vituo vya afya vya Makongolosi na Kambikatoto zimekwama kwenye mfumo tangu Septemba mwaka jana.

Alisema tatizo hilo limekuwa likiathiri utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa wilaya hiyo na kwamba endapo zitatoka watamaliza tatizo hilo na wananchi watakuwa wanapata huduma zinazostahili.

"Hili la wajawazito kukaa muda mrefu kwenye vituo bila kuhudumiwa tutalishughulikia kwa sababu lipo ndani ya uwezo wetu na tutahakikisha tunawahudumia vizuri lakini hili la vifaa tiba tunaomba mtusaidie," alisema Dk. Andrew.

Alisema wakati mwingine huwa wanawakusanya pamoja kwa lengo la kuwapatia elimu ya uzazi wao wenyewe na wenza wao ili walee vizuri mimba.

Akitoa maagizo ya chama, MNEC Mwaselela aliagiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chunya kushughulikia tatizo la mfumo ili fedha zitoke na vifaa tiba vinunuliwe ili kuondoa tatizo la wananchi kuchelewa kupata huduma.

Alisema endapo watashindwa wanatakiwa kupeleka taarifa kwenye chama ili kiwasiliane na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.



Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Shabani Mdende (kushoto), akizungumza na wadau wa usafirishaji Mkoa wa Mbeya hivi karibuni, kuhusu namna ya kuboresha huduma kwa wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dampo la maji machafu lawakera wakazi Wanging'ombe

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WAKAZI wa vijiji vitatu katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe wameiomba serikali kuliondoa dampo linalotiririsha uchafu kwenye vyanzo vya maji na kusababisha kuumwa magonjwa ya mlipuko ikiwemo matumbo.

Wakizungumza na Nipashe, wamesema wanapata shida juu ya uwepo wa dampo hilo ambalo lipo mlimani na linatumiwa na Halmashauri ya Mji Makambako na kuiomba serikali kulifunga kwa sababu limewekwa kimakosa.

"Hili dampo lipo juu ya mlima kabisa tunavyanzo viwili vya maji viko jirani kabisa, wananchi wanatumia maji haya, mifugo inatumia maji hayo na kiukweli na uhalisia wananchi wanapata shida ya kuumwa kupitia dampo hili kutiririsha maji mvua zinaponyesha, takataka zote zinatoka na kuingia kwenye mito," alisema Jerad Daudi Mwenyekiti wa Kijiji cha Itengelo.

Daudi alisema waiomba serikali kulisimamisha hilo dampo kwa sababu linahatarisha maisha yao.

Naye Innocent Bonifance alisema kuwa kero juu ya dampo hilo ni ya muda mrefu na licha ya kulalamika hakuna hatua zilizochukuliwa.

Michalina Mkumba alisema: "Kwa kweli hili dampo linatuletea shida tunapata ugonjwa wa matumbo kwa sababu tunachota maji kwenye visima kwa sababu hatuna bomba kwa hiyo inavyonyesha mvua maji yanatiririka yanakwenda kwenye mito miwili ambayo tunatumia".

Diwani wa Kata ya Saja, Andrew Mangula, alisema dampo hilo ni tatizo la muda mrefu.

"Tumekaa vikao kadhaa vya Baraza la Madiwani la Wanging'ombe, tumezungumzia sana habari hii lakini tumekaa vikao halali vya kamati tukizungumzia athari za dampo hili dampo hili liko juu ya mlima," alisema Mangula.

Mangula alisema kuwa kuhusu dampo hilo kuna sintofahamu ambayo inashangaza kwa sababu licha ya malalamiko ya wananchi lakini haliamishwi.

"Watu wa NEMC (Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira walipofika hapa walijiridhisha kwamba dampo hili linaathari kwa binadamu na wakatoa waraka wakasema ni kweli wanayoyazungumza kwamba dampo hili linaathari kwa binadamu hususani Kijiji cha Itengelo, Igomba, Saja na kijiji kilichopo kata ya Uhenga," alisema Mangula.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Onesmo Liandala alisema baraza la madiwani la halmashauri hiyo haibariki uwepo wa dampo hilo kwa sababu linahatarisha maisha ya wananchi.

# Wajasiriamali walia ubovu miundombinu, mitaro mitaani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJASIRIAMALI wanaofanya shughuli zao katika eneo la Ituha Kata ya Ilomba jijini Mbeya, wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara za mitaa na mitaro katika maeneo yao ili kunusuru bidhaa zao zisisombwe na maji.

Walitoa kilio hicho juzi walipozungumza na Nipashe kuhusu kero mbalimbali zinzowakabili, walisema mvua ikinyesha bidhaa zao zinasombwa na maji yanayotiririka kutoka milimani kutokana na kutokuwepo kwa mitaro imara. Mmoja wa wajasiriamali hao, Lucy Mbwiga alisema eneo hilo halina barabara yoyote iliyochongwa vizuri na hivyo mvua ikinyesha maji yanasambaa kwenye makazi na kwenye biashara zao hali ambayo inawasababishia madhara.

Alisema bidhaa zao huwa zinasombwa na maji na kusababisha hasara na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu hiyo ili kunusuru biashara zao.

"Kwa sasa mvua ikianza kunyesha tunafunga biashara zetu na kurudi nyumbani, maji huwa yanasambaa eneo lote hili na hata hii barabara yetu huwa haipitiki kabisa," alisema Lucy.

Naye Edga Siabale aliomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuwasaidia kuboresha barabara hizo akidai kuwa zipo chini ya wakala huo.

Alisema kipindi hiki ambacho mvua inanyesha barabara zimeharibika kiasi kwamba watu wanaomiliki magari wanapata hasara kwa magari yao kuharibika mara kwa mara kutokana na ubovu wa barabara hizo.

Alisema maeneo mengine ya jiji hilo barabara ziko katika hali nzuri isipokuwa katika kata hiyo ambayo alisema inachangia kwa kiasi kikubwa mapato ya halmashauri.

Alisema katika eneo hilo ndiko mchanga unachimbwa na baadhi ya mazao yanalimwa na hivyo halmashauri inakusanya ushuru ambao ungetumika kuboresha miundombinu.

"Tumesahaulika sana katika eneo letu hili, tunachangia kwa kiasi kikubwa mapato ya halmashauri, hapa kuna ushuru wa mchanga na mazao kama viazi tunalipa, tunaomba sana TARURA watusaidie," alisema Siabale.

Diwani wa Kata ya Ilomba, Tonebu Chaula alikiri kuwepo kwa tatizo hilo la ubovu wa miundombinu ya Barabara ambapo alisema wanaendelea kupambana ili kutatua kero hiyo.

Alisema alipofuatilia aliambiwa kuwa barabara hizo hazijasajiliwa na TARURA na hivyo akaahidi kupambana ili kuhakikisha zinasajiliwa na kuanza kufanyiwa marekbisho.

Kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya, miundombinu mingi ya barabara imeharibika na kusababisha mawasiliano kukatika kabisa kwa baadhi ya maeneo.



## Waingia makubaliano ya upatikanaji huduma bora za afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MFUKO wa Huduma za Afya Zanzibar na Taasisi ya Pharm -Acess zimeingia makubaliano ya ushirikiano ili kuimarisha utendaji kazi katika mfuko huo.

Akizungumza jana katika hafla hiyo iliyofanyika Ofisi za ZSHF Michenzani Mall visiwani hapa, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Yaasin Ameir Juma alisema makubaliano hayo yatasaidia kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote.

Alisema makubaliano hayo ni pamoja na kushirikiana katika kusajili sekta isiyo rasmi na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha na kushirikiana katika maeneo ya kitaalamu ili kuimarisha mfuko huo na kuendelea kutoa huduma bora kwa Wazanzibari.

"Ushirikiano kati yetu na taasisi ya Pharm -Acess ni ya muda mrefu kuanzia kuusarifu mfuko huu. Hadi kufikia hapa tulipo tunaendelea kushirikiana ili kuendeleza utoaji wa huduma bora za afya kwa jamii" alisema Yaasin.

Akizungumzia suala la kuendelea na usajili wa makundi mengine, alisema hivi karibuni wanatarajia kuanza usajili wa wanachama wa sekta binafsi ambapo Pharm-Acess wamekuja kuunga mkono ili usajili huo kukamilika kwa haraka.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Taasisi ya Pharm-Acess, Heri Marwa, alisema kuwa ushirikiano uliopo kati yao ndiyo umesaidia uwepo wa mfuko huo na kuwaomba wananchi kuutumia mfuko ipasavyo ili kupata huduma bora na za uhakika.

Aidha alisema kuwa taasisi hiyo ikifanya kazi na sekta mbalimbali za serikali ikiwemo afya ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea.

Hata hivyo alisema watahakikisha kuwa watu ambao hawana uwezo wanaishi katika mazingira magumu wanapata huduma kupitia mfuko huo ili kuboresha afya zao.

# Wanaougua malaria Zanzibar wafikia 5,300

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wagonjwa wa malaria visiwani Zanzibar mwaka huu wamefikia 5,300, Kisiwa cha Unguja kikiwa na wagonjwa 5,020, Pemba 280.

Takwimu hizo zimetolewa jana na Ofisa Afya ya Jamii wa Wizara ya Afya, Mwinyi Khamis na kueleza kuwa kati ya wagonjwa hao 11 wamefariki.

Alisema kwa mwaka 2023 wagonjwa 36 wa malaria walifariki kati ya wagonjwa 18,174 walioripotiwa visiwani Zanzibar, Unguja ikiwa ni 17,567 na Pemba 607.

Mwinyi alisema wanaume wanaongoza kwa kupata ugonjwa huo, huku waendesha bodaboda wakiwa ni wengi kutokana na mazingira wanayokaa katika biashara hiyo.

Alisema wanaume wengi wamepata malaria kwa sababu ya kukaa nje muda mrefu hasa nyakati za usiku na kushambuliwa na mbu ikilinganishwa na wanawake.

"Asilimia 66.7 ni wanaume waliopata malaria ikilinganishwa na wanawake ambao walikuwa asilimia 33.3 na wagonjwa 334 walilazwa hospitali kwa kupatiwa matibabu" alisema.

Alisema wilaya za Unguja na Pemba zimeathiriwa na ugonjwa huo ambapo Wilaya ya Mjini Unguja inaongoza na makundi yalioathirika ni waendesha bodaboda, mafundi ujenzi hasa wanaojenga nyakati za usiku, wanaokwenda kumbi za starehe na watazamaji wa mpira nyakati za usiku na umri ulioathirika ni miaka 15 hadi 45.

Alisema mambo yaliyosababisha kurudi kwa kasi kwa ugonjwa wa malaria Zanzibar ni mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo mvua na kutengeneza mazalia ya mbu kwa kutuwama kwa maji.

Pia alisema sababu zingine ni mienendo ya watu kusafiri baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, baadhi ya wanajamii kutotumia afua za kujikinga na malariai kiwemo matumizi ya vyandarua wakati wa kulala.

Sababu zingine ni kuchelewa kufika vituo vya afya kwa wenye dalili ya malaria, kutokubadilisha tabia na kutomaliza dozi ya malaria kwa wagonjwa wanaopatiwa matibabu.

Akizungumza kuhusu maradhi ya mlipuko, Meneja wa Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya, Hamad Magarawa, alisema uchafu wa mazingira pia ni moja ya chanzo cha kuongezeka kwa magonjwa hao ikiwemo maji ya taka yaliosheheni bila ya kuhifadhiwa.

"Maradhi mengi ya mlipuko yanaibuka kwa sababu ya uchafu, bado waandishi wa habari tunahitaji kutumia kalamu zenu vizuri katika kutoa elimu"alisema Magarawa.

Akizungumzia kuhusu ugonjwa wa corona, Magarawa alisema ugonjwa bado upo na kwa kuwa Zanzibar ni nchi ya kitalii bado kuna mwingiliano kati ya wageni.

Alisema watu 483,940 wamepatiwa chanjo ya corona Zanzibar hadi Desemba 2023 ambao walipatiwa dozi ya mwanzo bila ya kupata chanjo ya nyongeza (kubusti) ambapo wanaume ni asilimia 40 na wanawake asilimia 59 ya waliochanja chanjo ya awali.

"Chanjo ya Uviko -19 inashuka nguvu ya uhalisia ya kukulinda kutoka miezi sita hadi mwaka mmoja na badala ya hapo kama hujapata chanjo ya ziada ugonjwa unaweza kukupata,"alisema.

Alisema kila mwezi Zanzibar inawagonjwa wapya wa ugonjwa huo ambapo kwa Desemba mwaka jana wagonjwa 25 waliripotiwa na Januari mwaka huu zaidi ya wagonjwa 10.

Hivyo aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo ikiwemo kuchanja chanjo ya ziada kwa wale ambao walichanja chanjo ya awali na wale ambao hawajachanja.



Ofisa Afya Jamii Kitengo cha kupambana na malaria kutoka Wizara ya Afya, Mwinyi Khamis akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa malaria ambapo kuanzia Januari mwaka huu tayari watu 11 wameshafariki dunia. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wavuvi waipa angalizo serikali meli zinazopiga nanga Malindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAVUVI katika Wilaya ya Mjini wameitaka serikali kuwa makini na wamiliki wa meli zinazopiga nanga katika eneo la Bandari ya Malindi, wakisema wananya uchafuzi wa mazingira ikiwemo kumwaga mafuta baharini na kuharibu matumbawe.

Wavuvi hao walisema hayo wakati wa kikao cha pamoja kilichowashirikisha wavuvi na kamati za uvuvi za Wilaya ya Mjini kilichafanyika katika Soko la Malindi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Walisema baadhi ya wamiliki wa meli hawachukui tahadhari juu ya uwepo hifadhi ya bahari na kumwaga mafuta baharini hali inayoleta athari kwa viumbe wa baharini.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uvuvi Malindi, Hemed Said Ali alisema kuchafuliwa kwa bahari kwa kumwaga mafuta ni moja ya uchafuzi wa mazingira na kuwataka wasimamizi wa maeneo hayo kuwa makini na kuzifuatilia meli zote zinazo piga nanga katika eneo hilo ili kuepusha athari.

Katibu wa Uvuvi, Uhifadhi ya Mizingani, Omar Kombo, aliishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuwapatia boti za uvuvi ambazo zinahimili kuvua kina kikubwa cha maji ili kuongeza uzalishaji.

Alisema boti zinazazotolewa kwa wavuvi ni ndogo na hazina uwezo wa kuhimili mawimbi ya bahari zinapokwenda kuvua kwenye kina kirefu cha maji, hivyo waliomba kupatiwa boti hizo pamoja na vifaa vya uvuvi ili kuzitumia kwa shughuli zao.

Hata hivyo aliomba kupatiwa fedha za mgawo zinazokusanywa kupitia hifadhi ya bahari ya CHABAMCA ili wafanya kazi hao watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

Mweka hazina wa wavuvi hao eneo la Malindi, Pandu Makame Pandu aliiomba serikali kuwapunguzia kodi za mabanda ya kuhifanyia samaki aina ya papa kutoka Sh. 450,000 hadi Sh. 120,000 kwasababu kodi iliyowekwa na shirika ni kubwa kulinganisha na mapato ya wavuvi.

"Tulikuwa tunalipa Sh.70,000 kwa mwezi laki baada ya kumaliza ukarabati wa majengo yetu ya kuhifadhia papa Shirika la Nyumba la Taifa limetutaka tulipe Sh. 450,000 lakini hatuna uwezo wa kulipa," alisema.

Akitoa ufafanuzi juu ya malalamiko yaliyotolewa na wavuvi hao, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Sudi Hamed alisema wanatarajia kutoa fedha za mgawo kwa wakuu wa taasisi ya hifadhi ya CHABAMCA.

Akizungumza kuhusu wavuvi wanaofanya uvuvi haramu alisema wataendelea kutoa elimu kwa wavuvi ili kuondosha changamoto zinazojitikeza.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaabani Ali Othman alisema watafanya marekebisho ya leseni za uvuvi ili kuondoa changamoto zinazowakabili wavuvi.

Akizungumzia kuhusu mipaka ya hifadhi na visiwa alisema suala hilo litafanyiwa kazi na wavuvi wana haki ya kufanya shughuli zao katika maeneo ya bahari.

Aidha aliwataka wavuvi na wakuu hao wa taasisi kushirikiana na watendaji wa wizara hiyo ili kuondosha changamoto zinazojitokeza kati ya wavuvi na wakuu wa taasisi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**YONAH DAUD SHILINGI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1223/0075/2016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIMALI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/18231/2024**

**DEED POLL ON CHANGE OF THE NAME**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS**
**ORDINANCE ACT (CAP 117) R.E 2002**

BY THIS DEED I. the undersigned REHEMA KIVAMBE ABEID of MOROGORO Tanzania DO HEREBY Absolutely renounce and abandon the use of my former name RAHMA ABEID KIVAMBE as appears in my citizen Identity card No. 19990903332140000111.

AND IN PURSUANCE of such a change of name as aforesaid I HERE DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records deed and instrument in writing and in all actions and proceedings and transaction and upon all occasions whatsoever use and sign the name of REHEMA KIVAMBE ABEID as appears in my Birth certificate and my Academic Certificates in lieu of RAHMA ABEIF KIVAMBE renounce as aforesaid.

AND I DO HEREBY authorize and request all persons to designate and address me by the name of REHEMA KIVAMBE ABEID as it appears only.

IN WITNESS WHEREOF I hereunder signed my assumed of REHEMA KIVAMBE ABEID in the day and in the manner hereinafter appearing.




**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

BY THIS DEED, I SHABANI ALI AMANZI a citizen of Dar es Salaam in the united Republic of Tanzania, DO HEREBY wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my other names of MMETUKA A. SHABAN which appears on my PPF ID Card and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former names, the name of SHABANI ALI AMANZI.

For the purpose of evidence of such determination, I hereby DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deeds, documents and other writings and in all actions, suits and legal proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of SHABANI ALI AMANZI as my name, which appears in my citizenship identity card issued by NIDA bearing ID No. 19510511-14125-00001-25 in lieu of and in substitution for my former names of MMETUKA A. SHABANI

AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of SHABANI ALI AMANZI.

IN WITNESS WHEREOF I have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old names which I used interchangeably, by my new name of SHABANI ALI AMANZI.




## KUPOTEA KWA KADI BAJAJI

**ROBINSON MELECK NGUMBUKE** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **TVS KING,** Yenye usajili namba: **MC 961 CJV, CHASSIS NAMBA: MD6M14PA7K4K01838** na **ENGINE NAMBA: AK4KK4201747.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MKO/RB/16/2024**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA**
**WILAYA YA KARATU UTHIBITISHO WA USIMAMIZIWA MIRTHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 01 LA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**ZACHARIA MNYASA**
**LWEYEMAHO..................................MAREHEMU**
**NA**
**MONIKA HAFLA ZACHARIA............................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu.

Mapingamizi yote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnano au kabla ya tarehe 7 February, Mwaka 2024.

**Imewasilishwa Karatu leo tarehe 8 Mwezi January, 2024.**



HON. S.S.MUSHUMBUSI
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA KARATU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BABY GIDEON SHOO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye usajili namba **T 687 CEN, CHASSIS NAMBA: SCP103275868** na **ENGINE NAMBA: 1SZ0836264.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/2470/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA

**JANETH JACOB GOLLIAMA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE550814** iliyotolewa uhamiaji makao makuu **DAR ES SALAAM** tarehe **25/1/2023.** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/17929/2024**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Hamas yabainisha vipengele vilivyovunjwa na Israel

●Ni katika mapendekezo ya kusitisha vita

**GAZA,** PALESTINA

VYANZO vya ndani vya Hamas vimebainisha vipengele vilivyovunjwa wakati wa makubaliano kati yao na Israel, ikiwa kama masharti ya usitishaji vita huko Ukanda wa Gaza, ikiwamo kilichosema kuwa, awamu ya kwanza, kundi hilo ingewaachilia wafungwa wa Israel, wakiwemo wanawake, watoto, wazee, na wagonjwa, badala ya wafungwa 1,500.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Hamas jana, wafungwa hao wangejumuisha Wapalestina 500 waliopata vifungo vya maisha na vifungo virefu pamoja na wanawake, watoto na wazee wote wanaoshikiliwa katika magereza ya Israel.

Kipengele kingine kilikuwa ni angalau malori 500 ya misaada na mafuta kupelekwa kila siku katika maeneo yote ya Ukanda wa Gaza, kurejeshwa kwa Wapalestina waliokimbia makazi yao, kuhakikishiwa uhuru wa kutembea kati ya kaskazini na kusini mwa Ukanda huo, na kufunguliwa kwa vivuko.

Lingine ni pendekezo la angalau nyumba 60,000 za muda na mahema 200,000 yaruhusiwe kuingia Ukanda huo wakati wa awamu ya kwanza, uidhinishaji wa ziada wa mpango wa kujenga upya nyumba, vifaa vya kiuchumi na vifaa vya umma ambavyo viliharibiwa ndani ya miaka mitatu.

Hamas pia iliwataka walowezi kuacha kuvamia msikiti wa Al Aqsa na kwamba hali katika msikiti wa Al Aqsa irejee jinsi ilivyokuwa kabla ya 2002.

Katika hatua nyingine Ofisa wa Hamas Muhhamad Nazzal, alibainisha kuwa pande tano ikiwamo Qatar, Misri, Uturuki, Russia na Umoja wa Mataifa, zimechaguliwa kuwa wadhamini ikiwa makubaliano ya mapatano na Waisraeli yatatimia.

"Tunatarajia mazungumzo kuanza. pindi inapoanza, vizuizi vyovyote vinaweza kutatuliwa njiani kufikia makubaliano ya mwisho ambayo tunaweza kuweka alama na kuvuka," alisema Nazzal.

Pia ilielezwa kuwa ofisa huyo alijibu kwa ukali alipoulizwa kuhusu maoni ya Rais wa Marekani Joe Biden, na kudai kwamba pendekezo la kundi lake lilikuwa juu kidogo.

"Hatutarajii rais wa Marekani kuja na kauli bora zaidi. Ana upendeleo kabisa na alikuwa sehemu ya vita vilivyoanzishwa huko Gaza. Alitoa kifuniko cha kisiasa na kisheria kwa Waisraeli na ameunga mkono hatua zote za Waziri Mkuu wa taifa hilo Netanyahu.

"Walifanya kazi bega kwa bega kwa kutoa msaada wa kijeshi na kifedha. Tunatarajia utawala wa Marekani kuja na uamuzi wa mwisho Je, wako tayari kwa vita kuendelea? Au wanataka usitishaji vita wa kudumu?," alisema Nazzal.

**ALJAZEERA**

# Jaji Uganda ateuliwa Makamu wa rais ICJ

**KAMPALA,** UGANDA

JAJI wa Mahakama Kuu ya Uganda Julia Sebutinde ameteuliwa kuwa makamu wa rais wa Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) iliyoko Hague, nchini Uholanzi.

Jaji huyo hivi majuzi alizua utata katika jumuiya ya kimataifa alipotoa uamuzi dhidi ya hatua za dharura zilizoombwa na Afrika Kusini dhidi ya Israel kuhusu vita vya Gaza.

Aidha, serikali ya Uganda ilijitenga na maoni pinzani ya jaji huyo, ikisema hawakilishi msimamo wa nchi hiyo ya Afrika Mashariki katika mzozo huo.

Alikuwa jaji wa pekee katika jopo la wanachama 17 wa ICJ kupiga kura dhidi ya hatua zote sita zilizopitishwa na mahakama ya ICJ katika uamuzi ulioamuru Israel ichukue hatua ya kuzuia vitendo vya mauaji ya halaiki inapopambana na wanamgambo wa Hamas katika Ukanda wa Gaza.

Pia ilielezwa kuwa Sebutinde alikuwa mmoja wa majaji wawili pekee waliotoa hukumu zilizopingana huku 15 wakipigia kura hatua za dharura ambazo zilishughulikia mengi ya yale ambayo Afrika Kusini iliomba katika kesi hiyo.

Ilibainishwa kuwa kulikuwa na maoni mengi ya ukosoaji kwenye mitandao ya kijamii, huku wengine wakishangaa ni kwa nini alichagua kutokuwa na huruma zaidi na kesi ya Afrika Kusini.

Licha ya hayo, mahakama ya ICJ juzi ilitangaza kwamba jaji Sebutinde alichaguliwa kuwa makamu wa rais kwa miaka mitatu, katika kile kinachoonekana kuwa kura kubwa ya imani.

**BBC**




Waandamanaji Senegal wakipaza sauti zao juu ya kupinga uamuzi wa kuahirishwa kwa uchaguzi mkuu mchini humo. **PICHA MTANDAO.**

# Sintofahamu upinzani ukipinga Kuahirishwa uchaguzi Senegal

**DAKAR,** SENEGAL

UPINZANI Senegal umelaani uamuzi wa bunge kuahirisha uchaguzi wa rais kwa miezi 10 na kueleza kitendo hicho kuwa ni mapinduzi ya kikatiba, ambacho wachambuzi wanasema kinalitumbukiza taifa hilo la Afrika Magharibi katika mzozo mbaya wa kisiasa.

Ilielezwa jana kuwa wabunge walio wengi wa chama tawala walipitisha hoja ya kuahirisha uchaguzi wa rais hadi Desemba 15 baada ya mjadala mkali na mvutano uliotokea Jumatatu ndani ya bunge na kuwalazimu polisi kuvamia kikao chao na kuwaondoa baadhi ya wabunge wa upinzani.

Pia ilielezwa kuwa kwa sauti moja wabunge waliidhinisha mabadiliko hayo yanayomruhusu Rais Macky Sall ambaye muhula wake wa pili unatarajiwa kumalizika Aprili mwaka huu, kubaki madarakani hadi pale atakayechukua nafasi yake kuapishwa.

Babacar Mbaye, amabaye ni mbunge wa upinzani alisema hakuna neno kwenye kamusi linaloweza kutafsiri hatua yao, isipokuwa ni neno la kuongeza muda wa muhula wa rais.

"Walipotoa hati ya hoja walituambia uchaguzi unaahirishwa hadi Agosti 25. Polisi walivamia na kutuondoa ili waweze kupitisha mabadiliko hayo ya katiba. Sasa uchaguzi unafanyika Desemba 15. Kwa hivyo hivi sasa tuko chini ya utawala wa kimabavu wa mwaka mmoja wa Rais Macky Sall. Tunatoa wito kwa wananchi kujitokeza na kuonyesha wakati umefika wa kutetea demokrasia," alisema Mbaye.

Mtaalamu wa masuala ya katiba nchini Senegal Prof. Babacar Gueye, anakosoa uwamuzi huo akilieleza shirika la habari la AFP kwamba ni ukiukaji wa misingi ya kidemokrasia na ni tukio la hatari sana ambalo halijawahi kutokea nchini humo.

"Kilichotokea jana ni tukio la kipekee la hatari, na hatari sana kwa demokrasia. Kesho rais anaweza kusimama, siku ya mkesha wa uchaguzi Desemba 15, na kurudia kitendo hicho hicho, na kubuni mazingira sawa na kusema kuna hatari ya kuzuka vurugu baada ya uchaguzi wa rais kuahirishwa tena kwa muda usiojulikana," alisema Gueye.

Aliongeza kuwa hawatakubali nchi yao ambayo imetajwa kama kitovu cha demokrasia Afrika itumbukie kwenye utawala wa kimabavu.

Wabunge kutoka chama cha Rais Sall ambao wameshindwa kukubaliana juu ya mgombea wa kiti cha rais aliyechaguliwa na rais mwenyewe, waliamua kuunga mkono pendekezo hilo.

Naye, Mbunge wa Moussa Diakate ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya sheria inayounga mkono serikali alieleza kuwa, Rais Sall alisema atatumikia mihula miwili na ameshikilia ahadi yake, akisisitiza kuwa hiyo isitafsiriwe kama njama ya kutaka kubaki madarakani.

Hata hivyo ilielezwa kuwa ghasia zilitokea nje ya bunge tangu Jumatatu lakini inaripotiwa kwamba Jumanne hali imekua ni tulivu kukiwepo na idadi kubwa ya polisi wa kupambana na ghasia kwenye njia za kuelekea bungeni ili kuzuia maandamano.

**VOA**

# BIASHARA UTD WAZAWADIWA NG'OMBE NA MKUU WA MKOA

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda ameizawadia timu ya Biashara United, ng'ombe mmoja baada ya kuzoa pointi saba ugenini kati ya tisa kwenye michezo mitatu mfululizo iliyocheza ya Ligi ya Championship dhidi ya Pamba FC, Copco na Stand United.

Mwishoni mwa wiki, Biashara United ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Stand United kwenye uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga, kabla ya mchezo huo Biashara ilitoka kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Pamba FC kwenye uwanja huo huo na baadae kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya Copco kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Ng'ombe huyo alipelekwa kwenye makao makuu wa klabu hiyo na msaidizi wa Mkuu huyo wa Mkoa, Yusuph Kuwaya na kukabidhi katika hafla fupi iliyohudhuriwa na viongozi pamoja na wachezaji wa timu hiyo.

Mjumbe wa Bodi wa klabu hiyo, Mbaraka Forogo, alimshukuru Mkuu wa Mkoa na kusema zawadi hiyo imeleta chachu ya kujituma kwao viongozi na wachezaji katika azma yao ya kuhakikisha wanarejea tena kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Alisema ng'ombe huyo atasaidia kupatikana kwa chakula kwenye kambi ya timu hiyo na kuongeza morali kwa wachezaji wao.

"Ni heshima kubwa kupewa zawadi kama hii na Mkuu wa Mkoa, ni mara chache sana hutokea na huu ni utashi wake kama mzazi na kama mlezi wa timu hii," alisema Forogo na kuongeza,

"Kimsingi tunahitaji michango ya wadau mbalimbali kuweza kuiendesha timu yetu katika mbio harakatizetu za kurejea ligi kuu, Mkuu wa Mkoa amefanya kwa sehemu yake na kututia moyo, milango ipo wazi kwa watu wengine," alisema Forogo.

Aidha, kwa upande wake kwa niaba ya wachezaji wenzake, Nahodha msaidizi wa timu hiyo, Babilas Chitembe alisema wachezaji wenzake wamefurahi kupata zawadi hiyo na inaonyesha jinsi gani Mkuu huyo wa Mkoa yupo karibu nao.

Biashara inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 43, ikizidiwa kwa uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa na Pamba FC iliyo nafasi ya pili kwa pointi kama hizo, wakitanguliwa pointi moja tu na vinara wa ligi, Ken-Gold inayoongoza ikiwa na pointi 44.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dar es Salaam, wakicheza mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaama kaqma walivyokutwa na mpiga picha juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *TPBRC yajipanga kuwainua mabondia wanawake nchini*

**Na Shufaa Lyimo**

KAMISHENI ya ngumi za kulipwa Tanzania (TPBRC) imeweka mikakati kwa mwaka huu 2024 kuwainua zaidi mabondia wanawake.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Kamisheni hiyo George Lukindo amesema kuwa mpaka sasa mabondia wa kike wapo 100 tu nchi nzima tofauti na mabondia wanaume ambao wapo zaidi ya 1000.

"Tumekuwa na changamoto ya mabondia wa kike, wapo wa chache tofauti na wanaume, sasa sisi kama kamisheni ya ngumi za kulipwa Tanzania tunataka kila pambano kubwa litakalokuwa linafanyika lazima liwepo pambano moja la wanawake," alisema Lukindo.

Alisema wanawake wana uwezo mkubwa isipokuwa wanashindwa kufika mbali kutokana na kutokujua njia sahihi za kupita ili kufikia mafanikio kama wanayoyapata mabondia wanaume.

"Mwaka huu tutashirikiana na waandaaji wa mapambano mbali mbali ili mapambano makubwa ya kuwania mkanda kwa upande wa wanawake litakalofanyika hapa nchini lazima kuwepo na mapambano ya wanawake," alisema.

Aidha, aliwataka vijana wa kike kujitokeza kwa wingi kujiunga na kujifunza mchezo huo ambao utawapa mafanikio makubwa kupitia vipaji vyao.

Pia alisema, TPBRC wapo kwenye mchakato wa kuona kila mkoa unakuwa na Chama cha mchezo wa ngumi za kulipwa ili kuupeleka mbele zaidi mchezo huo.

"Tunataka kila mkoa hapa nchini unakuwa na Chama cha ngumi za kulipwa kwa viongozi wa mikoa husika kufanya vikao na wadau mbali mbali kuwahamasisha kuutangaza mchezo wetu," alisema Lukindo.

## Ni 'vita' ligi ya wanawake leo

**Na Saada Akida**

LEO ni kama vita ya timu mbili zinazokimbizana kileleni mwa msimamo wa ligi kuu ya wanawake ambapo Simba Queens na JKT Queens zote zitakuwa kwenye viwanja viwili tofauti kusaka pointi tatu muhimu.

Simba Queens wanaoongoza ligi wakiwa na pointi 22, leo watakuwa ugenini kukabiliana na Geita Gold Queens kwenye uwanja wa Nyankumbu wakati JKT Queens wanaoshika nafasi ya pili wakiwa na pointi 21 wenyewe watakuwa nyumbani kwenye uwanja wa Meja Jenerali Isamihyo kukabiliana na Ceasiaa Queens ya Iringa.

Michezo hiyo miwili inatarajiwa kukoreza mbio za kuwania usukani wa ligi kuu ya wanawake ikiwa tayari michezo saba imeshachezwa.

Simba Queens wamepata nafasi ya kukaa kileleni baada ya JKT Queens waliokuwa wanaoongoza ligi hiyo kukumbana na adhabu ya kupokonywa ponti tano nnaSimba kupewa pointi tatu baada ya kubainika maafande hao kutofika kwenye uwanja uliopangwa kucheza mchezo wao dhidi ya Simba Queens.

Adhabu hiyo kwa JKT Queens ilitolewa na Kamati ya Soka la Wanawake ambapo kwa kutumia kanuni ya 18:45 iliipa Simba Queens ushindi wa mabao matatu nan pointi tatu huku ikitumia kanuni ya 32.1 – 3 ya toleo la mwaka 2023 kuikata pointi tano.

Mbali na mechi hizo mbili, pia leo kutakuwa na michezo mingine ambapo Bunda Queen wataumana na Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Karume mkoani Mara, Baobab Queens wenyewe watacheza na Amani Queens uwanja wa Jamhuri, Dodoma na Alliance Girls wenyewe watakaribisha Yanga Princess kwenye uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

## Kuogelea waenda fainali za Dunia Qatar

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji wanne wa timu ya Taifa ya kuogelea kinaondoka leo kwenda Doha nchini Qatar kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Dunia ya mchezo huo yanayoanza Februari 11 mpaka Februari 18.

Wachezaji wanaounda kikosi hicho ni pamoja na Natalia Ladha, Amylia Chali, Michael Joseph pamoja na Prince Alimanya .

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha mchezo wa kuogelea Tanzania (TSA), Inviolata Itatiro, alisema malengo yao ni kwenda kuipeperusha vema bendera ya Taifa kwa waogeleaji kupata matokeo mazuri.

Inviolata alisema watapa nafasi ya kushiriki mkutano mkuu Shirikisho la Mchezo wa Kuogelea duniani ambapo ajenda kubwa itakuwa namna ya kuendeleza mchezo huo duniani.

Aidha, alisema mashindano hayo yatawasaidia wachezaji kupata uzoefu na uelewa wa michezo ya Kimataifa pia yatawaongezea uwezo wa kuogelea.

"Mashindano hayo yatatusaidia kupima viwango vya waogeleaji wetu kwenye anga za Kimataifa, hivyo watapata faida mbali mbali, alisema Katibu huyo.

Kikosi hicho kinatarajia kurejea nchini Februari 19 mara baada ya kumalizika kwa mashindano haya.

## ZISIKUPITE

### FERNANDEZ KUONDOKA CHELSEA

KIUNGO wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 23, anafikiria kuondoka Chelsea mwaka mmoja tu baada ya kujiunga na klabu hiyo kwa euro milioni 121 akisaini mkataba wa miaka nane na nusu. (*FootballTransfers.com*)

### WACHEZAJI HAWAMTAKI POCHETTINO

WACHEZAJI wa Chelsea wamelalamika kuwa mbinu za ufundishaji za Mauricio Pochettino na wasaidizi wake ni finyu, huku wachezaji wapya waliowasili wameonesha majuto juu ya mikataba yao ya muda mrefu. (*Athletic*)

### ALONSO ATAJWA LIVER

LIVERPOOL imefanya mawasiliano na kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso baada ya uamuzi wa Jurgen Klopp kuwa ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu. (*Footmercato*)

### MAN KUSAJILI VIJANA

MANCHESTER United inataka kuwekeza zaidi kusajili vijana wakati wa majira ya joto, huku mshambuliaji wa Crystal Palace mwenye umri wa miaka 22 kutoka Ufaransa, Michael Olise na mlinzi wa Everton mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite wakilengwa kusajiliwa. (*inews*)

### SAVIO BADO MAN CITY

KLABU ya Manchester City bado haijamsajili winga wa Brazil, Savio mwenye umri wa miaka 19, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Girona ya Hispania kutoka Troyes ya Ufaransa, lakini mazungumzo yamefanyika na timu hiyo ina matumaini ya kumsajili. (*ESPN*)

### HODGSON KUTEMWA

KLABU ya Crystal Palace inafikiria mustakabali wa Roy Hodgson kama kocha wa klabu hiyo, kwani wanataka kutafuta mbadala wake. (*Times*)

### GREENWOOD ATAKIWA ATLETICO

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mason Greenwood, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Getafe, amewekwa kwenye orodha ya Atletico Madrid ya washambuliaji ambao wanafikiriwa kusajiliwa msimu wa joto. (*Telegraph*)

### MAN UNITED YALENGA NYOTA

MANCHESTER United italenga wachezaji ambao wanaingia mwaka wa mwisho wa mikataba yao msimu huu wa joto na wanaweza kuzungumza na mchezaji kama vile kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 28, mshambuliaji wa Lille ya Canada, Jonathan David mwenye miaka 24, na kiungo wa kati wa Nice, Mfaransa, Khephren Thuram mwenye miaka 22. (*ESPN*)

### CHIESA AFUATILIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inamfuatilia mshambuliaji wa Juventus na Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26. (*HITC*)

### HAALAND HAONDOKI CITY

MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23, hana mpango wa kuondoka Manchester City huku kukiwa na uvumi kuwa anaweza kujiunga na Real Madrid. (*Football Insider*)

### CAZIER-DUBERRY KUBAKIZWA

ARSENAL inataka kumbakisha winga wao, Amario Cozier-Duberry mwenye umri wa miaka 18, huku Newcastle United, Ajax, Borussia Dortmund, Wolves na Anderlecht zote zikimtaka. (*Fabrizio Romano*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO ANATAMANI KURUDI TENA CHELSEA

**LONDON,** England

● ● ● Mreno huyo angependa kurejea kwa kipindi cha tatu kuifundisha timu hiyo kama wataamua kuachana na....

JOSE Mourinho angependa nafasi ya kurejea kwa kipindi cha tatu kama kocha Mku wa Chelsea, kwa mujibu wa ripoti ya ESPN.

Kocha wa sasa wa The Blues, Mauricio Pochettino amejikuta kwenye presha kubwa baada ya kushuhudia timu yake ikirudi kwenye nusu ya mwisho ya jedwali la Ligi Kuu ya England, huku baadhi ya mashabiki wakiimba jina la Mourinho ndani ya dimba la Stamford Bridge wakati Chelsea ilipolala mabao 4-2 na Wolves mwishoni mwa wiki.

Mourinho, ambaye kwa sasa hana kazi baada ya kufukuzwa AS Roma mwezi uliopita, amezungumza vyema kuhusu Chelsea tangu alipoondoka England, na kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, "angependa" fursa ya kurejea Stamford Bridge kwa mara nyingine tena.

Mourinho angefurahi kurejea Chelsea kwa sababu za kibinafsi.

Nyumba ya familia yake iko umbali wa mita 200 tu kutoka Stamford Bridge na inafahamika kuwa watoto wake bado wanaishi London pamoja na mkewe.

Kama matokeo, kurejea Chelsea kutamvutia Mourinho, lakini inabakia kuonekana kama Todd Boehly na Behdad Eghbali wataendelea kumuamini Pochettino, ambaye alidai Jumanne kupokea ujumbe chanya wa kuungwa mkono na wamiliki hao baada ya kipigo cha Wolves.

Mourinho alijiunga na Chelsea kwa mara ya kwanza mwaka 2004 kama uteuzi wa kwanza wa Roman Abramovich, na alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu akiwa na The Blues hao kabla ya kutoelewana na mmiliki na kumfanya aondoke 2007.

Baada ya kuziongoza vyema Inter Milan na Real Madrid, Mourinho alirejea Chelsea mwaka wa 2013 na, akiwa na mastaa kama Diego Costa na Cesc Fabregas upande wake, alileta taji moja zaidi kabla ya kuondoka mwishoni mwa 2015.

Tangu kuinoa Chelsea, Mourinho pia amezinoa Manchester United na Tottenham Hotspur, lakini hajawahi kuficha mapenzi yake kwa The Blues, akiwataja kama "Chelsea yangu" katika mahojiano na Sky Sports msimu uliopita wa joto.

"Chelsea watakuwa Chelsea daima," alisema. "Chelsea itakuwa kubwa siku zote na nyumba yangu ipo umbali wa mita 200 kutoka uwanjani hivyo nataka kuendelea kusikiliza sauti ya furaha na mafanikio, nina uhakika itakuwa hivyo.

"Bila shaka, muunganisho wangu wa Kiingereza ni Chelsea. Hivyo ndivyo ninavyoona mambo, kama kocha wa Chelsea baada ya vipindi viwili vya miaka sita."

# SON AOMBA RADHI KOREA KUTOLEWA KOMBE LA ASIA




**DOHA,** Qatar

HEUNG-Min Son aliomba radhi kwa mashabiki baada ya Korea Kusini kutupwa nje ya michuano ya kombe la mataifa ya Asia na Jordan, juzi.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klinsmann ndicho kilichokuwa kinapewa nafasi kubwa ya kuelekea nusu fainali hiyo, lakini walikutana na kichapo cha 2-0 ndani ya Uwanja wa Ahmed bin Ali nchini Qatar, Yazan Al-Naimat na Musa Al-Taamari wakifunga mabao hayo kipindi cha pili.

Korea Kusini walikuwa na asilimia 70 ya umiliki wa mchezo, lakini walipiga mikwaju nane pekee iliyolenga bao ikilinganishwa na 17 iliyopigwa na wapinzani wao.

Ni mara ya kwanza kwa Jordan kutinga fainali ya Kombe la Asia na matokeo yanafanywa kuwa ya kuvutia zaidi kwa kuwa kwa sasa wanashika nafasi ya 87 katika viwango vya ubora vya FIFA duniani.

Kwa Son, bado inasikitisha zaidi katika hatua ya kimataifa baada ya kumaliza kama mshindi wa pili katika mashindano ya 2015.

Nahodha huyo wa Korea Kusini mwenye umri wa miaka 31, alisema baada ya mechi: "Sijui niseme nini. Samahani sana.

"Wachezaji walijitahidi sana. Nasikitika sana mchezo uliisha hivi kimakosa.

"Mashabiki walionyesha sapoti kubwa kwetu, nasikitika kwamba hatukuweza kufanya kama mashabiki wetu walivyotarajia.

"Nitajitahidi zaidi ili timu ya taifa ikue zaidi siku zijazo, tena samahani sana."

Kocha wa Korea Kusini, Klinsmann aliongeza: "Nimesikitishwa sana, nina hasira kwa sababu tungefanya vyema zaidi usiku wa leo (juzi).

"Hakika sitatembea usiku huu nikitabasamu. Lakini kuna sababu za kupoteza mchezo huu na tunapaswa kukubali hilo."

Son sasa atarejea Tottenham kwani Kombe la Asia halina mechi ya mtoano ya kutafuta mshindi wa tatu - na fowadi huyo anaweza kupatikana kwa ajili ya mechi ya nyumbani ya Ligi Kuu huko London Kaskazini dhidi ya Brighton wikendi hii.

Kwa upande wa Jordan, watamenyana na Iran au taifa mwenyeji Qatar katika fainali siku ya Jumamosi.

# Misri yateua kocha pacha

**CAIRO,** Misri

MISRI imewateua ndugu pacha kuinoa timu yao ya taifa ya soka, huku Hossam Hassan akichukua nafasi ya ukocha Mkuu na Ibrahim Hassan kama mkurugenzi wa timu.

Chama cha soka cha Misri kilisema Hossam ambaye ni mfungaji bora wa muda wote wa nchi hiyo akiwa na mabao 68, atamrithi kocha raia wa Ureno, Rui Vitoria, ambaye alitimuliwa Jumapili baada ya timu hiyo kukosa matokeo mazuri kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON.

Misri, ambayo ina rekodi ya kutwaa mataji saba ya AFCON, ilishindwa kushinda mchezo wowote katika michuano ya 34 ya michuano hiyo na ilitolewa na DR Congo kwa mikwaju ya penalti katika hatua ya 16 bora.

Hossam mzaliwa wa Cairo aliisaidia Misri kutwaa mataji matatu kati ya hayo.



Alichezea zaidi klabu ya Al Ahly ya mji wa nyumbani kwake, pia akicheza PAOK ya nchini Ugiriki na timu ya Uswisi, Neuchâtel Xamax. Pia alichezea klabu nyingine kadhaa za Misri kabla ya kustaafu soka mwaka 2008.

Tangu wakati huo alifundisha klabu nyingi za Misri na timu ya taifa ya Jordán.

Ibrahim, beki wa zamani, pia aliwahi kuichezea Misri na kuongozana na kaka yake katika klabu mbalimbali.

Shirikisho la Misri lilikuwa limesema linatafuta kocha wa kigeni kuchukua mikoba ya Vitória na kocha Mfaransa, Herve Renard alikuwa akipewa nafasi kubwa ya kuchukua nafasi hiyo.

Vitória, ambaye aliteuliwa kuwa kocha wa Misri kwa mkataba wa miaka minne mwaka 2022, alishindwa kupata matokeo bora kutoka kwa timu hiyo.

Mafarao hao walitoka sare katika michezo yao yote ya makundi ya AFCON kwa sare ya 2-2 dhidi ya Msumbiji, Ghana na Cape Verde kabla ya kufungwa kwa mikwaju ya penalti na Congo.

Baada ya kumpoteza Mohamed Salah kutokana na jeraha la msuli katika mchezo wa pili wa kundi dhidi ya Ghana, na kipa namba moja, Mohamed El Shenawy aliyeteguka bega kwenye mchezo dhidi ya Cape Verde, shirikisho la Misri lilitoa sadaka ya ng'ombe katika jaribio la kutafuta bahati kwa timu hiyo.

## Timber arejea kikosini Arsenal

**LONDON,** England

ARSENAL imemuongeza beki Mholanzi Jurrien Timber kwenye kikosi chao cha Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha pili cha msimu huu huku akikaribia kurejea baada ya kupata jeraha baya.

Timber alijiunga na Arsenal kutoka Ajax kwa takriban pauni milioni 38 wakati wa majira ya joto, lakini alipata jeraha baya wakati wa mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu England, baada ya kufanyiwa upasuaji, aliachwa kwenye orodha ya kikosi cha Ulaya kwa hatua ya makundi.

Lakini Timber sasa amerejea kwenye kikosi, huku Mikel Arteta akimpa nafasi ya juu ambayo iliachwa na Lino Sousa aliyejiunga Aston Villa Januari.

Makadirio ya awali ilikuwa mchezaji huyo pengine angekuwa nje kwa kipindi cha miezi saba hadi tisa na angerejea Machi, lakini sasa imeonekana nyota huyo atarejea pungufu ya muda huo.

Arsenal itamenyana na Porto katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini mechi hiyo itakaribia haraka sana kwa Timber. Mechi ya kwanza imepangwa kufanyika Februari 21, na marudiano Machi 12.


Iwapo Arsenal wataendelea, wanaweza kumtumia Timber kwenye robo fainali, ambayo inatarajiwa kuanza Aprili 9 na kumalizika siku nane baadaye.

"Kwa bahati mbaya, hilo ni jeraha la muda mrefu," alisema Arteta.

"Anafanya vizuri sana lakini bado yuko mbali na kuwa fiti kufanya mazoezi na timu, au kitu cha kushindana na timu kwa hivyo hatutarajii atarejea hivi karibuni."

Timber alianza msimu kama beki wa kushoto wa Arsenal, kwa sababu ya kukosekana kwa Oleksandr Zinchenko, lakini jeraha lake la kutisha mwishoni mwa juma la ufunguzi wa msimu lililmlazimu Arteta kufanya mabadiliko.

Takehiro Tomiyasu ambaye ni mahiri amesaidia upande wa kushoto nyakati fulani, kama vile mlinzi wa kati Jakub Kiwior, lakini kurejea kwa Timber kunaongeza matumaini ya Arsenal.



HABARI MICHEZO

# KAPOMBE, KOUASSI VITA YA 'ASISTI' LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KROSI ya Shomari Kapombe iliyozaa bao la pili la Simba kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi juzi ikicheza dhidi ya Tabora United, imemfanya kufikisha pasi 'Asist' nne za mabao, akimkaribia kwa karibu kinara wa pasi hizo kwa upande wa mabeki katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Yao Kouassi wa Yanga mwenye pasi tano.

Katika mechi ya juzi ambayo Simba ilishinda mabao 4-0 kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous Chama alitoa 'Asist ' mbili na kusaidia timu yake kuibuka na ushindi huo mnene wakiwa ugenini.

Mpaka sasa kiungo wa Azam FC, Kipre Junior anaongoza kwenye orodha ya wachezaji waliotoa pasi nyingi za mabao akifanya hivyo mara sita akifuatiwa na Kouass na Kapombe.

Katika orodha hiyo pia yupo beki wa pembeni wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda ambaye naye ana asist nne akiwa mbele ya mchezaji mwenzake wa Azam, Paschal Msindo na nahodha msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein wenye asist tatu kila mmoja.

Wachezaji waliotoa asist mbili mpaka sasa wamo Cheikh Sidibe wa Azam FC, David Brayson wa Tanzania Prisons, Miraji Abdallan wa Coastal Union na beki wa kulia wa Yanga, Nickson Kibabage. Kibabage alifikisha asist ya pili, Jumatatu iliyopita, Yanga ilipoifunga Dodoma Jiji bao 1-0 lililowekwa wavuni na Mudathir Yahaya na kuiopa ushindi huo wa pekee.



Vijana wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaama juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Malindi SC yapanga kuzinduka leo*

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WEKUNDU wa Mji Mkongwe, Malindi SC wamejidhatiti kuanza kusaka pointi tatu kuanzia mchezo wa leo wa ligi kuu Zanzibar watakaocheza dhidi ya Ngome FC ili kuepuka kushuka daraja.

Malindi SC katika michezo 16 waliyocheza, wameshinda michezo minne pekee huku wakitoka sare michezo mitatu na kufungwa michezo tisa matokeo yanayowafanya kushika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 15.

Leo watakuwa na kibarua kigumu mbele ya Ngome FC kwenye mchezo utakaochezwa katika uwanja wa Mau A kuanzia saa 10:00 Alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Mohamed alisema wanaingia uwanjani leo wakiwa na lengo moya tu la kupata pointi tatu ili kuhakikisha timu hiyo inatoka katika mstari mwekundu wa kushuka daraja iliyopo sasa.

Alisema kupitia mchezo wao uliopita dhidi ya Kipanga FC wameweza kufanya maboresho kikosi chao hasa safu ya ulinzi ili kuhakikisha makosa yao waliyoyafanya kwenye michezo iliyopita hayajirudii.

Alisema safu yake ya ulinzi katika michezo iliyopita haikuwa sawa hali iliyopelekea kuruhusu magoli hivyo kitu kikubwa ambacho alikipa kipaumbele katika mazoezi ya timu hiyo ni safu yake ya ulinzi kuongeza umakini na ubunifu wa kiuchezaji pale wanaposhambuliwa.

"Tunashuka uwanjani lengo letu ni kupata alama tatu, alama ambazo tutaendelea kuzichanga ili kujiondoa katika nafasi hii ya chini tuliyopo sasa, nina matumaini makubwa tutafanikiwa," alisema Mohamed.

Aidha alisema kuwa mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa wanakutana na timu ambayo ina hali ngumu katika Ligi kama walivyo wao.

"Tunacheza na timu ambayo inaburuza mkia katika Ligi kuu ya Zanzibar, watakuja kwa lengo la kupambana na wao ili kuhakikisha wanapata alama tatu, na sisi lengo letu ni hilo hilo hivyo mchezo huu utakuwa mgumu pande zote"Alisema.

## Simba yashtuka, yamuandalia mkataba mpya Clatous Chama

INATOKA UK 24

wa miezi sita na yupo tayari kuongeza mkataba mpya.

"Suala la kuongeza mkataba hilo naamini lipo kwa uongozi wangu na uongozi wa timu, mimi nafurahia kuwepo Simba na kuwa sehemu wachezaji wanaoipambania timu," alisema na kuongeza,

"kama kutakuwa na jambo lolote naamini litajulikana, kwa sasa naipambania timu yangu na nimefurahi kuona tumepata ushindi wenye mechi mbili za ugenini, nina furaha kuchangia moja kwa moja mabao mawili na kufika malengo yetu ya kupata alama tatu katika mchezo dhidi ya Tabora United," alisema kiungo huyo.

## Gamondi: muhimu pointi tatu

INATOKA UK 24

dondosha pointi mbili.

Matokeo ya mechi hizo yameifanya kuendelea kuongoza ligi lakini kwa tofauti ya pointi mbili tu dhidi ya watani zao Simba wanaoshika nafasi ya pili wakiwa na pointi 32.

Kwa upande wake, Kocha wa Mashujaa FC Mohammed Abdallah 'Bares', alisema hawaigopi Yanga ila wanaiheshimu kwa kuwa ni timu kubwa na inaongoza ligi lakini wapo tayari kupambana.

"Wao watakuwa na wachezaji 11 na sisi hivyo hivyo, mchezo hautakuwa rahisi lakini hatutakubali kupoteza, tupo tayari kupambana kupata pointi," alisema Bares.



# Michezo

Nipashe

Alhamisi Februari 8, 2024




Mourinho anatamani kurudi Chelsea UK. 21

UZINDUZI...



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (kulia) akikata utepe kuzindua ofisi mpya ya Klabu ya Yanga Jangwani jijini Dar es Salaam jana, kushoto ni Rais wa klabu hiyo, Mhandisi, Hersi Said. **PICHA: JUMANE JUMA**

# Simba yashtuka, yamuandalia mkataba mpya Clatous Chama

**Na Saada Akida**

## ●●● Mkataba wa sasa wa Mzambia huyo unaenda ukingoni, viongozi wajifungia kujadili juu ya....

UONGOZI wa klabu ya Simba umeanza mchakato wa kumuongezea mkataba mpya kiungo wake Clatous Chama ambaye mkataba wake wa sasa unaelekea ukingoni.

**Simba ni kama imeshtuka kutokana na kiwango kizuri alichokionyesha mzambia huyo kwenye mechi ya juzi na hata katika fainali za kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON.**

Awali kulikuwa na taarifa kuwa kiungo huyo angeweza kuachwa mwishoni mwa msimu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo utovu wa nidhamu uliopelekea kusimamishwa kabla ya kusamehewa, lakini kiwango alichoonyesha katika mechi dhidi ya Mashujaa FC na juzi dhidi ya Tabora United, kimewafanya viongozi wa Simba na Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha kupagawa na kukaa chini kumuandalia mkataba mwingine mnono.

Katika mchezo wa juzi uliochezwa kwenye uwanja wa Ally Hassan Mwinyi mjini Tabora, kiungo huyo alichangia kwenye ushindi wa mabao 4-0 walioupata Simba huku mwenyewe akitoa pasi mbili za magoli.



Taarifa za uhakika kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema uongozi upo kwenye mipango ya kumuongezea mkataba mpya Ki-

awali kubakisha miezi sita tu kufikia tamati.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo alisema hatua ya kumuongezea mkataba nyota huyo ni baada ya mazungumzo ya pande zote likiwemo benchi la ufundi linaloongozwa na Abdelhak Benchikha na uongozi wa juu wa klabu hiyo.

"Suala la usajili lazima kocha ashirikishwe iwe nyota wapya au hata wale ambao mika-

iwemo Chama ambaye amebakiza miezi sita ili awe huru, uongozi tayari umeanza mchakato wa kumpa mkataba mwingine na tayari mazungumzo ya pande zote yameanza ukiwemo upande wa mchezaji," alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Alisema hivi karibuni mambo yakikamilika nyota huyo atasaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili juzi baada ya mchezo wao dhidi ya Tabora, Chama alisema yeye bado ni mchezaji halali wa Simba ana mkataba

INAENDELEA UK 23

# Gamondi: muhimu pointi tatu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo wakiikaribisha Mashujaa FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha wa Yanga Miguel Gamondi amesema kwake kwa sasa muhimu pointi tatu ili kuendelea kukaa kileleni mwa msimamo.

Timu hizo leo zitaumana kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi huku kila timu ikiwa na lengo la kuondoka na pointi tatu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Gamondi alisema wamefanya maandalizi kwa ajili ya mchezo wa leo kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo mazuri na kuendelea kuongoza katika msimamo.

Alisema ligi imefikia sehemu ngumu ambapo kila timu inapambana kupata pointi tatu hivyo wataingia kupambana kupata pointi tatu bila kujali idadi ya magoli.

"Lengo letu la kwanza ni pointi tatu, kwa sasa lazima tujue ligi imefikia kwenye ushindani wa juu, kila timu inapambana kupata ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri, ni vizuri kupata magoli mengi kwa sababu nayo yana faida yake, lakinikwanza ni kujihakikishia pointi tatu," alisema Gamondi.

Aidha, alisema anatambua mchezo wa leo hautakuwa rahisi kwa sababu ya wapinzani wao kutoka kupoteza mechi iliyopita na wanahitaji alama kama ilivyo kwao ili kujiweka kwenye mazingira mazuri katika mipango yao.

"Hii ratiba ni kwa timu zote, kikubwa ni kufanya maandalizi kwa ajili ya mchezo husika, haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya wapinzani wetu nao wamejipanga kuleta ushindani mkubwa, kikubwa ni kupambana kwa lengo la ushindi" alisema Gamondi.

Yanga inaingia uwanjani leo huku ikiwa na presha kutokana na upinzani walioupata kwenye mechi mbili zilizopita ambapo waliambulia pointi nne waki-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >